# Nipashe

Jumatatu Juni 28, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580625

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





**Rais** asisitiza tena kuchukua tahadhari ya maambukizi ya corona

UKURASA 2



**Vyama** 12 vyajitokeza kushiriki uchaguzi mdogo ubunge Jimbo la Konde

UKURASA 5

**Viungo 6 wanaoweza kuzihama klabu zao**

UKURASA 12 & 13

# Wengi wafunguka siku 100 za Rais Samia

• **Wataka** mifumo imara, mabadiliko ya sheria, Tundu Lissu amzungumzia...*Endelea ukurasa 2 & 3, 4*





Tundu Lissu


Togolani Mavura


Ummy Mwalimu


Abdulmajid Nsekela


Zitto Kabwe


Onesmo Ile Nguruma

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**CHONGOLO AONYA WANACCM KUELEKEA UCHAGUZI WA NDANI**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameonya...

UKURASA WA 7

**WANAWAKE UMAKI WATEMBELEA SERENGETI**

ZAIDI ya wanawake 200 wa Umoja wa Wanawake wa Kikristo wa Kanisa la...

UKURASA WA 7

**MENEJA ATEMWA KUONDOA WATU HIFADHINI BILA KIBALI**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amemsimamisha...

## Wauguzi matatani tuhuma za kudai wagonjwa rushwa

UKURASA 5

## Muswada wa bomba mafuta watua bungeni

UKURASA 5


**MICHEZO** NYOTA YANGA KUVUNA BIL. 4.9/- UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Wengi wafunguka siku 100 za Samia

**Na Salome Kitomari**

SIKU 100 za Rais Samia Suluhu Hassan kuwa madarakani, jana zilitikisa mtandaoni baada ya watu mbalimbali kuandika wanavyoridhishwa na utendaji kazi wake ikiwamo kuleta umoja wa kitaifa, kusimamia haki na uwajibikaji.

Katika kurasa za Twiter za viongozi na watu mbalimbali walionyesha jinsi wanavyoridhika na utendaji kazi wa Rais Samia, huku walioongea na Nipashe kwa njia ya simu wakitoa ushauri wa mambo ya kufanyika zaidi ili kuendelea kupaisha Tanzania kiuchumi ikiwamo kujenga mifumo imara ya kitaasisi.

Akizungumza na Nipashe kwa simu, Mtaribu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema ndani ya siku 100 amefanya kazi kubwa na kutatua matatizo yaliyopigiwa kelele kwa asilimia 50.

Akitoa mfano wa kero hizo, alisema ni watu kubambikiwa kesi, kuwa na mfumo mzuri wa masuala ya kodi, asasi za kiraia kuruhusiwa kuendelea na kazi zao ikiwamo kuzungumzia umoja wa kitaifa ambao anaufanya kwa kukutana na makundi mbalimbali huku akihimiza mshikamano na ujenzi wa taifa.

"Ndani ya siku 100 amehakikisha taifa linakuwa na mazingira mazuri ya watu kufanya shughuli zao, wafanyabiashara wameondolewa vikwazo, kuna uhuru wa vyombo vya habari na asasi za kiraia zinafanyakazi bila woga wala kufungiwa," alisema na kuongeza;

"Amezungumzia masuala ya corona kwa uwazi na kuboresha uhusiano wa kimataifa. Nafurahi kuwa yale yote yaliyokuwa na shida ameyafanyia kazi ndani ya siku 100."

Kwa mujibu wa Olengurumwa, utendaji kazi wake umeleta taswira chanya kwa watumishi wa umma na Watanzania kwa ujumla na kwamba makundi yote kwenye jamii yamepata faraja.

"Ombi letu haya yote hayawezi kudumu kama hakuna mifumo mizuri na imara ya kitaasisi. Tunataka kuona taasisi kama Mahakama, Bunge vikiwa imara pia vyombo vya ulinzi na usalama vifanye kazi zake kwa maadili na uwajibikaji wa haki," alisema na kuongeza;

"Kubwa na muhimu zaidi ni kuboresha na kufanya marekebisho ya sheria zilizopo ambazo ziliruhusu mambo yaliyotendeka ndivyo sivyo, tukibaki hivi maana yake kuna wakati tutarudi huko na haya mazuri yaliyofanyika hayataendelea, lazima tuwe na mifumo mizuri," alisema.

Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliandika "Rais Samia ametumia siku zake 100 madarakani kuimarisha serikali na chama chake na kurejesha uhuru wa watu."

Naye, Waziri wa TAMISEMI, Ummy Mwalimu, aliandika "Hakuna kama Mama. Hongera sana Rais Samia siku 100 za uongozi wako zimekuwa ni siku za vitendo zaidi katika kutatua kero za Watanzania mfano, kuweka mazingira mazuri ya elimu ya msingi na sekondari kwa watoto, kuboresha huduma za afya msingi na barabara."

Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, aliandika "Heshima kwa mama kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuongoza taifa letu. Tukiwa tunaangazia siku 100 za Mheshimiwa Rais Samia tuna kila sababu za kufurahia wimbo huu "Nani kama Mama!"

Naye, Msanii wa Bongo Flavor, Elias Barnabas, katika video maalum ya siku 100 za Rais Samia alisema; "Hakika kwanza najivunia kumpata mama, siku zote ni mwenye huruma akudekeaye na akuvishaye nepi hawezi kukutupa mkono kwa kukunyima chakula. Hongera mama, nchi unaiongoza vyema, mustakabali wa taifa lako unaendelea kuwa vyema, Watanzania tunakutegemea."

"Songa bila kusitia wala kupepesa macho, fanya majukumu yako vile uonavyo, tenda kazi yako kwa weledi wako kwa sababu sisi wafuasi wako na watoto wako tuko nyuma yako. Hongera mama! Siku 100 zenye matumaini, zenye mabadiliko chanya na mwanya mkubwa wa kuonyesha siri ya mustakabali wa kile unachotaka kukifanya na nia ya dhati kwenye taifa lako," aliimba katika baadhi ya beti.

Naye, Dk. Ellen Senkoro aliandika; "Pongezi nyingi kwa Rais wetu kwa uongozi mahiri. Ni fahari na mfano kwa wanawake na wasichana wa Kitanzania, Afrika na Dunia."

Naye, Balozi Togolani Mavura aliandika "Siku 100 za Rais Samia Suluhu Hassan ni siku 100 za dhahabu."

Naye, Mwenyekiti wa Umoja wa watoa huduma za gesi na mafuta Tanzania (ATOGS), Abdulsamad Abdulrashid, aliandika; "Siku 100 za Rais Samia ndani ya ofisi, mabadiliko, anapenda biashara, mkamilifu, mkarimu, mwenye maamuzi, mnyenyekevu, mwenye upendo na mpenda haki."




Kijana akiwa ameshika bango lenye ujumbe wa kumtakia Rais Samia Suluhu Hassan, Mungu amsaidie na kazi iendelee, katika barabara ya Ally Hasan Mwinyi eneo la St. Mbuyuni, mkoani Dar es Salam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# ...Asisitiza tahadhari dhidi ya corona

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesisitiza umuhimu kwa Watanzania kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona ambao upo nchini.

Aidha, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa mkoani Tanga kwenye Mkutano Mkuu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), aliwataka wananchi kuchukua tahadhari ya corona kikamilifu.

Naye, Paroko wa Kanisa Katoliki katika parokia ya Handeni mkoani Tanga, Padri Joseph Sekija, aliwataka waumini wake kutumia ushauri wa wataalamu wa afya, kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa huo.

Rais Samia katika ukusara wake wa Twiter aliandika "Nawasihi Watanzania wenzangu tuendelee kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa Korona (Uviko-19) kama tunavyoelekezwa na wataalamu wetu wa afya. Tunawe mikono kwa maji tiririka na sabuni, tutumie vitakasa mikono, tuvae barakoa na tusigusane gusane. Ugonjwa wa Korona upo."

Akiwa jijini Tanga, Makamu wa Rais, Dk. Mpango aliwaomba viongozi wa dini kuwahimiza wananchi kujilinda na kuchukua tahadhari kwa kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya.

"Ni muhimu kuvaa barakoa, kunawa maji tiririka na sabuni mara kwa mara, kutumia vitakasa mikono, lakini pia kukaa umbali kati ya mtu na mtu," alisisitiza.

Padri Sekija, aliwataka waumini wake kutumia ushauri wa wataalamu wa afya, kujikinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema hatua hiyo ni muhimu na ambayo ilielezwa kwa kina na Rais Samia, alipokutana na kuzungumza na maaskofu wa kanisa hilo, kupitia Baraza la Maaskofu Wakatoliki Tanzania (TEC), jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Akihubiri kwenye misa takatifu jana, Padri Sekija alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoathirika kutokana na mlipuko wa tatu wa maambukizi ya Corona, hivyo inawapasa waumini hao na wananchi wengine, kuchukua tahadhari.

Alisema uongozi wa kanisa hilo katika parokia ya Handeni, umeshachukua tahadhari, ikiwa ni pamoja na kuweka vyombo vya maji tiririka kwenye maeneo tofauti, kuhamasisha uvaaji barakoa hasa kwenye mikusanyiko ya watu na kupunguza safari zisizokuwa na ulazima.

"Mheshimiwa Rais Samia wakati akizungumza na maaskofu wetu kule TEC, ameelezea kwa kina kuhusu mlipuko wa tatu wa maambukizi ya virusi vya corona, ninawasihi ndugu zangu, tufuate ushauri wenye kutukinga dhidi ya maambuzi hayo," alisema.

Alitoa mfano kuwa katika ziara yake kutoa huduma za kiroho kwenye kigango cha Negero, alishuhudia baadhi ya wazee wakiwa hawana uelewa wa matumizi ya vitakasa mikono (sanitizer), na hivyo akahimiza kwa wenye uelewa kuendelea kuwaelimisha wasiojua zaidi kuhusu kinga dhidi ya corona.

"Waliponiona nina kichupa cha 'sanitizer' wengine wakafikiri nimebeba ugoro...ipo haja ya kuendelea kuelimishana zaidi na kuchukua tahadhali kwa vitendo, tujikinge dhidi ya maambuzi haya," alisema.

Hata hivyo, Padri Sekija alisema pamoja na kutumia kinga za kisayansi, ipo haja kwa Watanzania kuendeleza maombi kwa Mwenyezi Mungu, ili aiponye Tanzania dhidi ya maradhi hayo.

Padri Sekija alitoa mfano wa habari ya binti mmoja aliyeponywa ugonjwa wa kuvuja damu, baada ya kushika pindo la vazi la Yesu, na kwamba vazi hilo kwa hivi sasa linawakilishwa neno la Mungu na nguvu zake za uponyaji.

●**Imeandikwa na Salome Kitomari (DAR) na Mashaka Mgeta (Handeni)**

HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani (kulia), akizungumza jana na wafanyabiashara katika Mnada wa Ng'ombe wa Ipuli , Manispaa ya Tabora juu, kuchukua tahadhari ya kujikinga dhidi ya virusi vya Corona. **PICHA: VICENT TIGANYA**

# LISSU: Miezi 3 ya Samia kuna uhuru, watu wanapumua

**Na Elizabeth Zaya**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo(CHADEMA), Tundu Lissu, amesema kwa kipindi cha miezi mitatu tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, kuna uhuru, watu wanapumua na vyombo vya habari vinaandika vitu ambavyo vilikuwa haviwezi kuandika.

Lissu alitoa kauli hiyo jana wakati akihojiwa na televisheni moja nchini Kenya.

"Ni kweli kuna mabadiliko, tuna rais mpya, Samia Suluhu Hassan. Katika miezi mitatu ambayo amekuwa rais, ni kweli kuna mambo yamefanyika ambayo yako tofauti na miaka mitano iliyopita. Kuna uhuru, watu wameweza kupumua, sasa hivi kila mtu anapumua, magazeti na vyombo vyetu vya habari sasa hivi vinaandika vitu ambavyo vilikuwa havidiriki kuandika,"alisema Lissu.

Akijibu swali aliloulizwa kuhusu uzuri wa marais wastaafu, Lissu alisema kwa kuanza na awamu ya kwanza ya Mwalimu Julius Nyerere, yapo aliyoyafanya.

"Kizuri cha Mwalimu Nyerere, alijenga na alikuwa rais muda mrefu kuliko kiongozi mwingine yeyote, alikaa madarakani miaka 24, lakini pamoja na kukaa muda mrefu madarakani, aliachia kwa hiari na bila kuhusishwa na wizi au ufisadi au uchafuzi wa mali za umma," alisema na kuendelea:

" Aliondoka madarakani akiwa na mikono misafi, akiwa msafi kwenye masuala ya matumizi ya madaraka na mali za umma, huwezi kumtuhumu Mwalimu Nyerere kwamba alituibia, hakutuibia."

Kuhusu Rais mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, Lissu alisema aliirudisha nchi katika msingi mzuri uliosaidia kuokoa uchumi na pia ndiye aliyeleta mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Kuhus Rais wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa, Lissu alisema hakuvuruga mfumo wa vyama vingi na alidhibiti Idara ya Usalama wa Taifa kwa kutungia sheria ya kudhibiti mamlaka yake.

Kuhusu Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, Lissu alisema miaka 10 ya Kikwete itakumbukwa kwa kuimarisha Bunge, kuweka bunge hilo kuwa mubashara na alipanua demokrasia.

"Na katika kipindi hiki ndipo tuliona jinsi ambavyo bunge linaweza kuwa, lakini ni rais ambaye chini yake demokrasia ilipanuka, vyama vya upinzani kama CHADEMA vilipata nguvu kubwa sana," alisema Lissu.

**KATIBA MPYA**

Akizungumzia kuhusu vuguvugu lakudai Katiba mpya linalofanywa na chama chake, Lissu alisema hakuna namna yoyote ambayo chama kikuu cha upinzani kitaenda kwenye uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchagu (NEC) kama ilivyo kwa sasa.

**WANACHAMA 19**

Akizungumzia waliokuwa wanachama chake wakiongozwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa chama chake (BAWACHA), Halima Mdee na wenzake 18, Lisssu alisema anashangaa sababu watu hao kuendelea kuwapo bungeni wakati chama chao kilishawafukuza uanachama.

"Hawa 19 wanaoitwa wabunge, tumewafukuza uanachama, wako bungeni kwa nini, ili uwe mbunge au diwani au hata mwenyekiti wa kijiji au mtaa, lazima uwe mwanachama wa chama cha siasa na ukipoteza uanachama kwa mujibu Katiba, unapopoteza ubunge au udiwani automatic, hawa tumewafukuza kwenye chama, wako bungeni kwa nini?" alihoji Lissu.

"Na hili ni suala muhimu sana, kuna makosa makubwa ya jinai yamefanyika, kuna watu wamegushi nyaraka za kuwafanya hawa watu wawe wabunge, sheria ya uchaguzi ya Tanzania inasema hivi, ili mtu awe mbunge wa viti maalum anayewakilisha wanawake, lazima kwanza chama chake kipeleke majina ya hao walioteuliwa kuwa wabunge kwa NEC," alieleza na kuongeza:

"Sisi hatujawahi kupeleka jina hata moja kwa sababu tulijadiliana kwenye kamati kuu ya chama, tukasema kwamba hatukubaliani na uchaguzi, na hatutapeleka majina ya wabunge na hatutachukua pesa ya ruzuku ."

# PM: Miradi 93 imesajiliwa siku 100 za Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema katika kipindi cha siku 100 za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, imesajili miradi 93 yenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.6 ambayo itaingiza ajira zaidi ya 24,600 kwa vijana.

Alisema kuwa hatua hiyo inatoa alama kwa wawekezaji wa nje kwamba kwa sasa urasimu katika sekta ya uwekezaji unaendelea kupunguzwa maeneo ya usajili wa kampuni mwekezaji anapokusudia kuwekeza nchini.

Waziri Mkuu aliyasema jana alipofungua Kongamano la siku 100 za Rais Samia Suluhu Hassan, lililofanyika katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Alisema Rais Samia amefanya jitihada kubwa ya kuondoa tozo 232 zilizokuwa zinawakwaza wafanyabiashara. "Tozo hizi zimeondolewa ili kuwawezesha wafanyabiashara kufanya biashara zao hapa nchini."

Alisema katika kufanya kazi zake, Rais Samia ameendeleza uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi jirani na ametembelea nchi za Kenya, Uganda na Msumbiji kwa lengo la kuimarisha urafiki na mataifa ya jirani.

Vile vile, alisema Rais Samia ameendelea kupanga mipango ya ujenzi wa miradi mipya katika siku 100 za uongozi wake ikiwamo kuweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa reli ya kimataifa kipande cha kutoka Mwanza mpaka Isaka, ujenzi wa meli mpya nne na ukarabati wa meli kongwe moja.

Pia, katika kipindi cha siku 100 za uongozi wa Rais Samia ameanzisha mradi wa shule za sekondari za wasichana katika halmashauri zote nchini. Ametoa Sh. milioni 500 kwa kila jimbo kwa ajili ya kukarabati barabara ili kuboresha huduma za usafiri vijijini.

Akiongea katika Kongamano hilo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania, Eric Hamissi, alisema katika kipindi cha siku 100 mamlaka hiyo imepokea barua za pongezi kutoka katika kampuni kubwa za usafirishaji duniani ikiwamo ya Mediterranian na Mesina Line kwa uboreshaji wa huduma bandarini hapo.

Alisema kuwa katika kipindi cha robo ya mwisho kuanzia Aprili hadi Juni, mwaka huu wamekusanya Sh. bilioni 236.8 sawa na ongezeko la asilimia 14 ikilinganishwa na robo iliyopita ya kuanzia Januari hadi Machi, ambayo walikusanya Sh. bilioni 203.

Naye, Kamishna wa Uhamiaji nchini, Dk. Anna Makakala, amesema kuwa kwa kushirikiana na idara ya kazi wameanza kutoa vibali kwa kutumia mfumo wa kielektroniki ambapo katika kipindi cha kuanzia Mei, 2021 hadi sasa wametoa vibali 3,377 vya kazi ukilinganisha na vibali 2166 vilivyotolewa katika kipindi kama hiki kwa mwaka jana.


**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**COMMERCIAL CASE NO. 80 OF 2020**

**SAO HILL INDUSTRIES LTD ………………………….. PLAINTIFF**
**VERSUS**
**NIPO GROUP LTD ……………………………………. DEFENDANT**

**DECREE:**

**WHEREFORE**, the Plaintiff prays for judgment and decree against the defendant as follows: -

i. A declaration that the defendant has breached the terms of the Purchase Agreement executed between the Parties.
ii. An Order for payment of Tanzania Shillings Nine Hundred Only (Tshs. 940,554,800/=) as at 20th August, 2020 being outstanding amount due and owing to the Plaintiff for the purchase of the Poles supplied by the Plaintiff to the Defendant and refund for payment of CESS for the Poles.
iii. An order for payment of an interest at commercial rate of 17% per annum of the Principal amount from the date of default until the date of Judgment.
iv. An order that the Defendant to pay general damages to be assessed by the Court for breach of contract.
v. An order that the Defendant to pay interest of Decretal amount at Court rate of 32% per annum from the date of Judgment to the date of full satisfaction.
vi. Costs of this suit.
vii. Interest on the costs at Court's rate of 12% from the date of Judgment until payment in full.
viii. Any other order and relief as this Honourable Court may deem fit and just to grant.

This suit coming up for judgment on 18th day of June, 2021, before Hon. Dr. D.J. Nangela, Judge in the presence of Ms. Sumaiya Jaffar, Advocate for the Plaintiff and in absence of the Defendant.

**THIS COURT DOTH HEREBY ORDER THAT:**

a) This Court declares that the Defendant has breached the terms of the Purchase Agreement executed between the two parties.
b) The Defendant is hereby ordered to immediately pay the Plaintiff a total of TZS 940, 554,800/= being the outstanding amount due and owing to the Plaintiff for the purchase of Poles supplied by the Plaintiff to the Defendant and refund of payment of CESS for poles supplied.
c) The Defendant is ordered to pay the Plaintiff interest at Commercial rate of 14% per annum on the principal amount from the date of default until the date of judgment.
d) The Defendant is hereby ordered to pay general damages to a tune of TZS 5,000,000 for breach of contract.
e) The Defendant is hereby ordered to pay interest on the decretal amount at court rate of 7% per annum from the date of judgment to the date of full satisfaction.
f) Costs of this suit.

Given under my hand and the seal of the Court this day of 18th day of June, 2021.

Dr. D. Nangela
**JUDGE, HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
18th day of June, 2021
Extracted on 18th day of June, 2021

216332802




# Rais Samia adhihirisha wanawake wanaweza

**Na Mary Geofrey**

KWA wale ambao wana mashaka na mwanamke nataka kuwaambia niliyesimama hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nataka kurudia niliyesimama hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye maumbile ya kike," hii ni nukuu ya kijasiri ya kutambulisha uwezo wake kama mwana mama, aliyeshika madaraka makubwa ya nchi.

Nukuu huyo aliitoa Machi 22, katika hotuba yake wakati wa kutoa heshima za mwisho na kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Tanzania Dk. John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17, mwaka huu katika Hospitali ya Mzena, mkoani Dar es Salaam kwa maradhi ya moyo.

Kupitia kauli hiyo, Rais Samia aliinua tumaini jipya kwa Watanzania na wanawake wote wa ndani na nje ya nchi, kuwa wanawake wanaweza wakipewa nafasi.

Rais Samia na Hayati Magufuli, waliingia madarakani kwa tiketi moja mwaka 2015; Magufuli akiwa Rais na Samia Makamu wake.

Rais Samia katika hotuba hiyo aliendelea kujinadi; "Walinipa nafasi ya kuonyesha uwezo wangu na wanawake tunaweza, kwa miaka sita nilihudumu kama msaidizi wake (Magufuli)."

Baada ya kuendelea kukitumia kiti hicho kama mwana mama, Rais Samia ameonekana kuwa tofauti na mtangulizi wake huyo katika mambo kadhaa ikiwamo aina yake ya uzungumzaji inayomtambulisha kama mama.

Kila anaposimama kuzungumza na Watanzania, anatumia sauti ya uungwana zaidi katika kufikisha ujumbe huku akiwa mwepesi wa kuchukua hatua kitendo kinachomfanya kutambulika kama mama.

Aprili 22, mwaka huu, aliingia katika Bunge la Tanzania kuhutubia kwa mara ya kwanza kama Rais wa nchini.

"Hii ni mara ya kwanza kwenye historia ya taifa letu kupata Rais Mwanamke. Kwa sababu hiyo, ninajua, watakuwapo baadhi ya watu wachache wenye wasiwasi kwamba kutokana na jinsia yangu sitoweza kuyatimiza yote niliyoyasema hapa.


Rais Samia Suluhu Hassan, siku ya kula kiapo cha kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. **PICHA: MAKTABA**

"Nataka nitumie jukwaa hili kuwaondoa hofu kwamba kwanza, Mwenyezi Mungu hakuumba ubongo hafifu kwa mwanamke na ubongo wenye uwezo mkubwa kwa mwanamume," anasisitiza Rais Samia.

Katika kuwahakikishia Watanzania kwamba makuzi na umakini wa akili hutegemea jamii inayokuzunguka na shughuli unazokuwa nazo, anasema;

"Nataka nikuhakikishieni kuwa nimekuzwa kwenye jamii sahihi na kwamba nina uzoefu wa kutosha kwenye serikali na kwenye chama changu cha siasa cha CCM.

"Hivyo basi, ninajiamini kuwa ninao uwezo wa kuliongoza taifa hili. Pili, kazi hii sitoifanya peke yangu bali nitashirikiana na Watanzania wote. Wito wangu kwa Watanzania, tushirikiane, tushikamane na kuwa kitu kimoja katika kulijenga taifa letu.

"Binafsi naamini, tukiwa na upendo, mshikamano na kuheshimiana, na kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, tutaweza kufika kule ambako sote tunatamani tufikie."

Tangu Rais Samia aingie madarakani amefanya mambo yanayowafanya wanawake watembee kifua mbele na kujiamini kuwa wakipewa nafasi wataonyesha maajabu.

Amewapa nguvu na ari ya kuweza kuvunja vikwazo vyote vilivyowekwa na mfumo dume katika jamii.

Kwa mara ya kwanza Juni 8, mwaka huu, Rais Samia alikutana na wanawake nchini tangu alipoapishwa kuwa Rais wa Tanzania.

Akiwa katika mkutano huo, anaeleza kuwa, sheria na maazimio yameifikisha Tanzania katika mafanikio mengi makubwa kama uwiano wa jinsia katika vyombo vya uamuzi na ajira.

"Mafanikio makubwa yamepatikana katika eneo hili na mfano halisi ni mimi niliyesimama hapa, miaka 20, 25, 30 nyuma hatukuwa tukilitazamia hili, lakini leo imewezekana tuko hapa." anasema.

Anafafanua zaidi kuwa; "Idadi ya wanawake katika vyombo vya uamuzi imeongezeka, ikiwamo mabaraza yetu ya mawaziri, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lakini pia wakuu wa mikoa, makatibu wakuu na kadhalika."

Rais Samia anasema, wanawake wametoa mchango mkubwa kwenye shughuli za maendeleo, kuanzia wanawake waliotengeneza njia wakati wa ukombozi wa Tanzania, ukombozi wa kisiasa, lakini pia wanawake walioshiriki kuikomboa Tanzania kwenye ile nadharia kuwa mwanamke ni mtu wa pili.

"Tulieleweka, tukashirikishwa tukawa hapa, lakini pia wapo waliotutangulia na sisi tuliopo ambao sasa tunakomboana kiuchumi.

"Tumetunga sera na sheria pamoja na kuridhia na kutekeleza mikataba na maazimio mbalimbali ya kikanda na kimataifa ukiwamo mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kutokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake wa mwaka 1979 pia azimio la Beijing la mwaka 1995 na mkataba wa kimataifa wa haki zote za mtoto mwaka 1989," Anasisitiza Rais Samia.

Rais Samia amesisitiza kuendelea kutoa fursa mbalimbali kwa wanawake ili kufikia asilimia hamsini kwa hamsini.

**UTEUZI WA WANAWAKE**

Tayari Rais Samia amefanya uteuzi wa Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, kushika wadhifa huo akiwa mwanamke wa kwanza.

Kwa wafuatiliaji wa siasa za Bunge, Nenelwa alistahili kupewa wadhifa huo kabla hata Samia hajawa rais, lakini pengine jinsia yake au kutojihusisha kwake na makundi ya kisiasa ndani ya chama ilikuwa kikwazo kwake.

Katika mkutano alioufanya na wawakilishi wanawake Juni 8, mwaka huu mjini Dodoma, Rais Samia aliahidi kuwa, katika utawala wake amedhamiria kuongeza nafasi za wanawake katika vyombo vya juu vya uamuzi ili washiriki katika michakato ya haki na maendeleo.

Akitoa mifano, anasema kwamba katika orodha ya Makatibu Tawala mikoa 26, aliowateua tangu aingie madarakani, amewapa wanawake 12 nafasi ambayo ni sawa na asilimia 46 ya wateule wote.

Pia, anasema kwamba katika majaji 28 wa Mahakama Kuu aliowateua, majaji 13 sawa na asilimia 43 walikuwa ni wanawake. Kwa sababu hiyo, katika majaji wote 86 wa Mahakama Kuu, wanawake sasa wamefika 40.

Eneo pekee ambalo alisema lina changamoto kubwa ni kwenye ajira rasmi ambako alisema kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2017, katika ajira rasmi milioni tatu (3,014,106), wanawake waliopata nafasi ni milioni moja (1,107,900) tu sawa na asilimia 36.7.

Rais Samia anasema, takwimu zinaonyesha Tanzania ina wanawake wengi zaidi kuliko wanaume na hilo lingetakiwa kuakisiwa katika takwimu muhimu za kimaendeleo kama ajira, lakini wengi wa wanawake wamejiajiajiri katika sekta binafsi na isiyo rasmi ambako vipato vyake si vya uhakika.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha DODOMA Mkoa DODOMA**
**Shauri la madai No 86/2021**
**Jina la mdai ALENI JORO**
**Jina la mdaiwa FESTO NICODEMO**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa **FESTO NICODEMO DODOMA.**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba **MADAI YA PESA TASLIM** Tsh. 612,000.
Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 23/07/2021 saa 2:30 asubuhi. Kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na kuthibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo 14/06/2021.
216332102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha DODOMA Mkoa DODOMA**
**Shauri la madai No 56/2021**
**Jina la mdai ESTER RWECHUNGULA**
**Jina la mdaiwa ADOFU BAREBI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa **ADOFU BAREBI**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba **MADAI YA TALAKA.**
Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 10/07/2021 saa 2:30 asubuhi. Kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na kuthibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo 25/06/2021.
116332202

**KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI KIWANJA**

**NDUGU IMMACULATE AIDAN MBARUKU** anatangaza kupotelewa na hati ya Nyumba yenye **TITLE DEED PLOT NO. 6 BLOCK P** Eneo **AREA E HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA.**
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu yake.
Taarifa ya Polisi
**DOD/DOD/RB/316490/2021**
116332502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA KINONDONI**
**SHAURI LA MIRATHI NA 118 LA 2021**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**ESTHER WILSON NYONGOLE……………………MAREHEMU**
**WOLTRAM JOSEPH NYONGOLE…………………MWOMBAJI**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 08 Mwezi 07 Mwaka 2021.

**Hati hii imetolewa tarehe 25 Mwezi 06 Mwaka 2021.**
116332302

HABARI KITAIFA

# Vyama 12 kushiriki uchaguzi mdogo wa ubunge Konde

Na Christina Mwakangale

WAGOMBEA 12 wamechukua fomu za uteuzi kwa ajili ya kuwania ubunge kwenye uchaguzi mdogo wa Jimbo la Konde, Kisiwani Pemba, unaotarajiwa kufanyika Julai 18, mwaka huu.

Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Konde, Yasini Jabu Hamis, alisema wagombea hao wanatarajiwa kurejesha fomu kabla ya saa 10 jana jioni, kwa ajili ya uteuzi.

Wagombea waliochukua fomu ni wanaotoka Chama cha Mapinduzi (CCM), Civic United Front (CUF), Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo), Sauti ya Umma (SAU), National Convention for Constitution and Reconstruction- Mageuzi (NCCR-Mageuzi) na Tanzania Labour Party (TLP), Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Vyama vingine ni Demokrasia Makini, Chama cha Kijamii (CCK), United People's Democratic Party (UPDP), National Reconstruction Alliance (NRA) na Tanzania Democratic Alliance (ADA-TADEA).

Jimbo la Konde linafanya uchaguzi kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo, Khatib Said Haji. Uchaguzi huo unafanyika sambamba na kata sita za Tanzania Bara, ambazo ni Mbagala Kuu iliyopo Mkoa wa Dar es Salaam (Temeke), Ndirigish iliyopo Mkoa wa Manyara (Kiteto), Mitesa na Nchemwa zilizopo Mkoa wa Mtwara (Masasi na Newala), Gare iliyopo Mkoa wa Tanga (Lushoto) na Chona iliyopo Mkoa wa Shinyanga (Ushetu).

Kampeni kwa ajili ya uchaguzi huo zinatarajia kuanza leo hadi Julai 17, mwaka huu na uchaguzi unatarajiwa kufanyika Julai 18.

# Wauguzi wahamishwa kituo madai kuomba wagonjwa rushwa 90,000/-

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WAUGUZI wawili wa Kituo cha Afya cha Bwanga wilayani Chato mkoa wa Geita, wamehamishwa, kwa kutuhumiwa kuomba Sh. 90,000 kwa wagonjwa waliokuwa wamelazwa.

Wanadaiwa kuomba fedha hizo kwa wagonjwa ili kuitumia kama nauli kwenda kufuata damu katika vituo vingine vya afya kutokana na kituo kukosa huduma ya damu.

Wauguzi wanaotuhumiwa ni George Makoye na Godfrey Willison, ambao wanadaiwa kuchukua fedha hizo kwa ndugu wa wagonjwa.

Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Leonidas Felix, alisema baada ya kufanya uchunguzi walibaini kuwatoza wagonjwa Sh. 90,000 kama nauli waliyotumia kwenda kutafuta damu kwenye kituo kingine cha afya.

"Kufanya hivyo walikiuka kanuni na taratibu za utumishi wa umma, kwa sababu hata uongozi wa kituo hicho haukupewa taarifa," alieleza Felix.

Alisema wauguzi hao wamerejesha fedha hizo kwa wagonjwa. "Tayari wauguzi hao wamelipa faini na hawatashitakiwa tena kwa sababu kufanya hivyo ni sawa na kuwapa adhabu mara mbili,"alisema Felix.

"TAKUKURU tunaitaka mamlaka ya nidhamu iwahamishe wauguzi hao na iwapeleke katika vituo ambavyo havihusiki na damu salama," alisema Felix.

"Watu wakibainika na makosa, huwa tuna mambo mawili; kuwapeleka mahakamani au kuwachukulia hatua za nidhamu, lengo ni kutoa fundisho kwao na kwa watumishi wengine wenye tabia kama zao."

Felix, alisema wauguzi hao kwa sasa wameshamishiwa katika vituo vingine, ambavyo havina huduma ya damu salama.




Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo(wa pili kushoto), akiangalia moja ya bidhaa inayotengenezwa na wafungwa wanawake wa Gereza la Isanga, baada ya kumaliza kikao cha kusikiliza maoni mbalimbali ya wafungwa hao. Ziara hiyo imefanyika jana jijini Dodoma. **PICHA NA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

# Samia apeleka bungeni Muswada wa bomba la mafuta

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amepeleka bungeni, Muswada wa Sheria kwa hati ya dharura, unaohusu uwekezaji wa ujenzi wa mradi mkubwa wa bomba la mafuta ghafi, kati ya Tanzania na Uganda.

Muswada huo wenye lengo la kulinufaisha taifa na utajiri wa rasilimali zake, unalenga zaidi kuzuia unyonyaji kupitia mikataba mbalimbali isiyolinufaisha taifa kwa kiwango kinachotarajiwa, utajadiliwa na Bunge kwa hatua zake zote, Juni 30, mwaka huu.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliwatangazia wabunge mwishoni mwa wiki kwamba amepokea Muswada wa hati ya dharura kutoka kwa Rais, Samia Suluhu Hassan, akitaka washughulikie sheria ambazo ziko katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Namba 3 wa mwaka 2021.

"Ni muhimu kwa sababu ni sheria zinazorekebishwa zinazoendana na uwekezaji wa bomba la mafuta la kutoka Uganda, kwa ajili ya kukuza sekta mbalimbali ili tuweze kufanikisha uwekezaji huo kwenda vizuri bila matatizo yoyote.

"Na sisi wabunge, mnafahamu tunasapoti kabisa mradi huo. Kwa hiyo tutaushughulikia muswada huu kwa hatua zake zote katika kipindi hiki hiki cha Bunge, kabla hatujaondoka hapa. "Kwa hiyo muswada huo tutaujadili siku ya Jumatano, baada ya maswali, tukimaliza ndiyo Mheshimiwa Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa), atasimama kusoma hotuba ya kuahirisha Bunge hadi wakati mwingine."

Kwa Mujibu wa Ndugai, Muswada huo wenye sheria mbalimbali zinazohitaji marekebisho, umepelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria.

"Kwa sababu ni sheria mbalimbali zinagusa sekta mbalimbali za nishati, uchukuzi, barabara na kadhalika, nimeteua wabunge ambao wataungana na Kamati ya Katiba na Sheria, wakitokea kamati mbalimbali na wataanza kuushughulikia huo muswada," alisisitiza.

Aprili 11, mwaka huu Rais Samia na Yoweri Museveni wa Uganda, walitia saihi mkataba wa ujenzi wa bomba hilo lenye umbali wa kilomita 1,440, ambalo litagharimu Dola za Kimarekani bilioni 15.

Mradi huo wa bomba la kusafirishia mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Bandari ya Tanga, unajulikana kama East African Crude Oil Pipeline (EACOP).

**WATANO WAONGEZWA**

Ndugai, alisema ili kuulainisha muswada huo, ameteua wabunge kutoka Kamati ya Serikali za Mitaa, kwenda kuungana na Kamati ya Katiba na Sheria kulainisha muswada huo.

"Kuna maeneo yanagusa na bomba hili, sasa nimeteua wabunge kutoka Kamati ya Serikali za Mitaa ambao ni Humprey Polepole, Abdalah Chaurembo, Tunza Malapo, Denis Londo na Magreth Sitta. Hawa watajiunga na Kamati ya Katiba na Sheria ili kuweka sawa mambo haya," alisisitiza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili Yanga, Azam umulike Simba ilipoteleza kimataifa

**NI** rasmi Simba, Yanga na Azam zitaiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa kwa msimu mpya wa 2021/22 unaotarajiwa kuanza mapema Septemba, mwaka huu kwa mechi za hatua ya awali Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika kupigwa.

Msimu huu Tanzania Bara itaingiza timu nne; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika, nafasi hizo zikitokana na juhudi za Simba kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa, hivyo kuiongezea nchi pointi na kuwa miongoni mwa nchi 12 zinazoruhusiwa kuingiza idadi hiyo kwa msimu.

Kwa mujibu wa Kanuni za Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bingwa wa Tanzania Bara na mshindi wa pili atacheza Ligi ya Mabingwa, huku mshindi wa tatu na Bingwa wa Kombe la FA wakicheza Kombe la Shirikisho.

Lakini endapo ikitokea Bingwa wa Ligi Kuu, akatwaa tena ubingwa wa Kombe la FA, basi mshindi wa tatu na wa nne wa Ligi Kuu ndiyo watakaokwenda kucheza Kombe la Shirikisho Afrika.

Hivyo, kwa namna msimamo wa Ligi Kuu ulivyo hadi sasa, Simba ina nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa huo, huku Yanga na Azam zikiwa tayari zimejihakikishia kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao kutokana pointi zilizonazo kutoweza kufikiwa na timu yoyote zilizopo nyuma yao.

Lakini pia Simba na Yanga zimetinga fainali ya Kombe la FA, hivyo hiyo ni tiketi ya wazi kabisa kwa timu mojawapo itakayoibuka mshindi kushiriki michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani humu, inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Ingawa bado msimu wa 2020/21 haujamalizika huku dirisha rasmi la usajili likiwa pia halijafunguliwa, tayari klabu za Yanga na Azam FC zimeanza kuingia mikataba ya awali na wachezaji wapya, na kwa sasa zikisubiri tu dirisha hilo kufunguliwa ili kusajili mikata yao TFF. Kwa ujumla tunazisifu kwa kuchukua hatua mapema kwani tunaamini hadi kufikia hatua hii zikiwa zimebakiza takriban michezo mitatu kabla ya msimu kumalizika, zimeshaelewa maeneo ambayo zinapaswa kuyaboresha katika Vikosi vyao.


Lakini hatuna budi pia kuziasa kuwa makini zaidi katika mchakato huo wa usajili kutokana na majukumu makubwa ya michuano ya kimataifa yaliyopo mbele yao kuelekea msimu mpya utakaoanza Septemba, mwaka huu.

Ni wazi kwamba Yanga na Azam FC zilishuhudia namna Simba ilivyopambana katika michuano hiyo na upinzani mkubwa iliyoupata, hivyo kwa kuanzia kama kweli zimedhamiria kufika mbali, zinapaswa kusajili wachezaji wenye uwezo kama ama zaidi ya wapinzani wao hao.

Hakuna ubishi kwamba Simba kwa sasa nchini ni klabu pekee inayojengwa na wachezaji wenye viwango vya juu zaidi, lakini bado haikufanikiwa kupenya nusu fainali na hatimaye fainali, hivyo kipimo cha usajili kwa Yanga na Azam kuelekea michuano hiyo kinapaswa kuwa ama daraja la wachezaji wa sasa wa Simba au zaidi ya hapo.

Tunatambua kwamba kuzidiwa mbinu ndiko kulikoifanya Simba kuishia robo fainali na si suala la uwezo wa wachezaji pekee, ndiyo maana tunawataka wawakilishi wetu hao wa msimu ujao kuhakikisha wanasajili wachezaji wa daraja la juu zaidi wakati huu pia Simba nayo ikitakiwa kujiimarisha kwa kuongeza nyota wenye uwezo zaidi ya walionao.

Kadhalika, kuna uwezekano mkubwa kwa Biashara United ya Mara kupata nafasi ya kushiriki michuano hiyo ya CAF kutokana na pointi ilizo nazo kwenye msimamo wa Ligi Kuu katika nafasi ya nne waliyopo, hivyo nayo haina budi kuanza kumulika wachezaji wa daraja la juu, kwani lengo letu ni kutaka kuona msimu huu timu zote nne zinatinga hatua ya robo fainali ama zaidi ya hapo kwenye mashindano hayo ili kujikusanyia pointi nyingi zaidi na kushikilia nafasi yetu ya timu nne.




## Muungwana Lazima Nilonge

# Nafasi timu nne kimataifa ilindwe



Na Adam Fungamwango

**NI** rasmi sasa kuwa Tanzania itapeleka wawakilishi wanne kwenye michuani ya kimataifa msimu ujao. Ni baada ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kutangaza rasmi kupata taarifa hiyo kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

TFF imesema kuwa timu hizi nne zitapatikana kwa Bingwa wa Tanzania Bara na mshindi wa pili kucheza Ligi ya Mabingwa, huku mshindi wa tatu na Bingwa wa Kombe la FA wakicheza Kombe la Shirikisho.

Hata hivyo, inaweza kubadilika kama Bingwa wa Ligi Kuu, atatwaa tena ubingwa wa Kombe la FA, ambapo hapo sasa mshindi wa tatu na wa nne wa Ligi Kuu ndiyo watakaokwenda kucheza Kombe la Shirikisho.

Shukrani kwa klabu ya Simba ambayo kutokana na kutinga kwa hatua ya robo fainali, Tanzania imeongeza pointi zilizoifanya kuongezeka timu kutoka mbili hadi nne.

Ikumbukwe kuwa msimu uliopita Tanzania iliwakilishwa na Simba iliyocheza Ligi ya Mabingwa na kutinga hatua ya robo fainali na Namungo FC ikashikiri michuano ya Kombe la Shirikisho na kutinga hatua ya makundi.

Hii ilitokana na timu za Tanzania kuvurunda msimu wa 2019/20 na hakuna hata moja iliyofanikiwa kutinga hatua hata ya makundi.

Simba ilifanya vema kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu wa 2018/19, ilipotinga pia hatua ya robo fainali, Tanzania ikapata nafasi ya kuwakilishwa na timu nne, ambazo ni wenyewe Simba, Yanga, Azam na KMC.

Timu zote hizo hakuna iliyofanya vizuri hata moja, japo kutinga tu makundi. Sasa nafasi zimerudi tena.

Kwa bahati nzuri, timu za Simba, Yanga na Azam zinarejea tena kwenye michuano ya kimataifa, lakini kuna nafasi moja ambayo kwa mbali inaonyesha kuwa Biashara United inaweza kuipata.

Huu sasa ndiyo wakati wa timu za Tanzania kufanya tathmini ya kina kabla ya kwenda kucheza michuano hiyo migumu Afrika. Ni wakati wa kutorudia makosa ya msimu uliopita uliosababisha kurudishiwa timu mbili tu kama ilivyozoelekwa kwa muda mrefu.

Hivi karibuni, Katibu Mkuu wa zamani wa Yanga, Dk. Jonas Tiboroha, aliziasa timu zitakazofuatana na Simba kwenye michuano hiyo. Akitoa maoni yake kama mdau wa soka kuhusu timu zitakazokwenda kuiwakilisha Tanzania kwenye mechi za kimataifa, ziangalie kwanza Simba ni timu ya aina gani hapa nchini ambayo imekwenda hadi robo fainali ya Ligi ya Mabingwa, lakini ikashindwa kutinga hatua ya nusu fainali, ndipo nazo zitengeneze timu yenye kariba hiyo kama zinataka kweli kwenda kushindana.

> **Kwa bahati nzuri, timu za Simba, Yanga na Azam zinarejea tena kwenye michuano ya kimataifa, lakini kuna nafasi moja ambayo kwa mbali inaonyesha kuwa Biashara United inaweza kuipata.**

"Klabu zitakazokwenda kucheza kimataifa ziangalie Simba ni timu ya namna gani. Imefikia hatua ya robo fainali na ikashindwa kupenya hatua ya nusu fainali, hivyo nazo zinatakiwa kutengeneza timu inayofanana kiuwezo wa timu hiyo au zaidi kama zinataka kufanya vizuri, vinginevyo zitaishia hatua ya mwanzoni tu kutolewa na timu za Eswatini na Comoro kwa sababu zitakuwa hazijafanya vitu vya msingi kuijenga kwanza timu," akasema.

Akaongeza kuwa Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho ni michuano migumu ambayo inatakiwa kwanza kuwa na timu imara, kuwa na muda sahihi wa kujiandaa na si kujaribisha, lakini pia timu zinatakiwa kuwa vizuri kiuchumi, kwani ni michuano yenye gharama kubwa na kuna mambo yanahitaji pesa nyingi ili timu iwe salama na kukabiliana na baadhi ya vikwazo.

Kwa kuongezea hapo tu ni kwamba Simba bado ina wachezaji ambao wana uwezo wa kucheza michuano hiyo, hivyo itakachofanya ni kuongeza nguvu tu, lakini timu zilizobaki itabidi zijidhatiti kisawasawa. Kinachotakiwa kwenye michuano hiyo angalau kwa timu kama za Yanga, Azam ni kutinga hatua za makundi kwanza ili Tanzania iwe na uhakika wa kubakisha nafasi hizo kwa ajili ya misimu mingine.

Ile tabia ya kuondolewa kwenye hatua za awali au raundi ya kwanza iondoke inabidi sasa tuikwepe kama tunataka kubaki na nafasi hizo nne.

Timu za Tanzania zitakapoanza kuwa na tabia ya 'kuishi' kwenye hatua ya makundi kila mwaka, hapo ndipo tutakapoona kuwa soka letu limepanda na si kazi ya kuiachia timu moja kwa sababu msimu ambao inatolewa mapema, basi nafasi zinapungua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Chongolo aonya wanaCCM kuelekea uchaguzi wa ndani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ameonya tabia ya makundi ndani ya chama hicho kwenye chaguzi mbalimbali zitakazofanyika februari mwakani.

Chongolo alitoa onyo hilo juzi alipokuwa akifungua Kikao cha Baraza la Umoja wa wanawake wa CCM(UWT),jijini hapa.

Alisema tabia ya kutengeneza makundi na kusengenyana zimekuwa zikifanywa na watu wanaojitafutia nafasi katika chaguzi mbalimbali ndani ya chama.

"Mwakani mwezi februari tunaanza uchaguzi ndani ya chama kuna watu ambao wao hivi sasa wanajitengenezea miundombinu ya kupata nafasi na siyo kutengeneza miundombinu ya kukijenga chama,"alisema Chongolo.

Alionya jumuiya za chama hicho kuacha kutumia vikao vya mabaraza kujadili mambo binafsi na majungu bali zijadili mambo yenye maslahi kwa taifa.

Alisema kuwa mikutano inayofanyika ilenge kujadili namna ya kutatua kero mbalimbali zinazowahusu Watanzania ambao ndiyo wamekipa dhamana chama hicho kuongoza.

Pia, alisema tabia ya vikao vya mabaraza ya jumuiya hizo za chama kutumika kujadili mambo binafsi hayana tija na hayawezi kukisaidia.

"Unakuta watu wanajadili mwanamke fulani mfupi mwingine mrefu au mwingine mweusi mwingine mweupe au nani kaolewa jana, kama kaolewa inakuhusu nini? Jadilini 'issues' acheni kujadili mambo binafsi,"alisisitiza Chongolo.

Aidha, alisema chama kinakabiliwa na tatizo la kutokuwa na takwimu sahihi za idadi ya wanachama wake jambo ambalo linasababisha kushuka kwa makadirio kila mwaka.

"Tumekuwa na changamoto kubwa ya kutokuwa na kumbukumbu sahihi ya wanachama pamoja na kutokulipa ada za chama kwa wakati," alisema Chongolo.

Aliiagiza UWT, katika vikao vyake vya mabaraza kuweka ajenda ya mkopo wa asilimia nne kwa wanawake kuwa ya kudumu.

"Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya mikopo hii ya asailimia nne lakini nyinyi kama wanawake lazima mjue kila wilaya ni wanawake wangapi wamenufaika na kiasi gani kimetolewa."

"Lazima hii iwe ajenda yenu ya kudumu katika vikao kuna wilaya inatenga bajeti ya mikopo ya kinamama bilioni nne kiasi ambacho anashangaa kwanini kinamama waendelee kulia kuwa hawana mitaji, hivyo mnatakiwa kujadili ili kuwasaidia wanawake wenzenu,"alisema.

Aliwataka wabunge wanawake kuhakikisha wanasimamia fedha zinazotengwa na Halmashauri kwa ajili ya wanawake ili kujiendeleza kibiashara na kudhibiti zisiishie mikononi mwa wajanja.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (kushoto) akiagana na Askofu wa Kanisa la EAGT wilayani Iringa, Ezekiel Mkenda (kulia), juzi baada ya kuzungumza na waumini wa kanisa hilo ambapo alitoa tahadhari kwa wananchi kujikinga na ugonjwa hatari wa Corona. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wanawake UMAKI watembelea Serengeti kuhamasisha utalii

**Na Allan Isack,** SERENGETI

ZAIDI ya wanawake 200 wa Umoja wa Wanawake wa Kikristo wa Kanisa la Anglikana Tanzani (UMAKI), kutoka Dayosisi ya Dar es Salaam, wametembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, kwa lengo la kuhamasisha na kuutangaza utalii wa ndani na kuhamasisha wananchi umuhimu wa kutembelea vivutio hivyo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, wakati wa kupokea kundi la wageni hao, Kamishna Mwandamizi wa Mawasiliano, kutoka Shirika la Hifadhi za Taifa(TANAPA), Pascal Shelutete, alisema wanawake wa kanisa hilo wanatokea Dar es Salaam na wamekwenda hifadhini humo kutalii na kuhamasisha utalii wa ndani.

Alisema wanawake hao kutembelea Hifadhi ya Serengeti, ni jitihada zilizofanywa na TANAPA, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa utalii ili kuhamasisha na kuutangaza utalii wa ndani.

"Kundi la wanawake 205 lililopo hapa, wanatoka Kanisa la Anglikana, Mkoa wa Dar es Salaam, ni waumini wa Kanisa la Anglikana, wamekuja hapa kwa ajili ya suala zima la utalii wa ndani na watakuwa katika hifadhi hii kwa siku tatu," alisema Shelutete.

Alisema shirika hilo linatoa kipaumbele katika eneo la utalii wa ndani na wamejipanga kuendelea kuhamasisha makundi mbalimbali kwenda kutembelea Hifadhi za Taifa kujionea maajabu ya vivutio hivyo.

"Natoa wito kwa Watanzania wenzangu kutembelea hifadhi hizi zenye vivutio mbalimbali ambavyo Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu kuwa navyo hivyo tutumie fursa hii kuja kutembelea maeneo haya," aliongeza.

Ofisa Masoko kutoka Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Eugine Maliya, alisema ujio wa wanawake hao, ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la serikali kwa bodi ya utalii kukuza na kuutangaza utalii wa ndani.

"Bodi ya utalii tunaendelea kuhamasisha makundi mbalimbali hapa nchini, kuja kutembelea hifadhi zetu kwa kuwa itakuwa moja ya njia ya kujionea maajabu yanayopatikana hifadhini na namna Mwenyezi Mungu, alivyoibariki nchi ya Tanzania," alisema Malya.

Alisema kundi la wanawake hao, kutembelea hifadhi hiyo kutaongeza chachu na kuleta mwamko kwa makundi mengi kwenda kutembelea vivutio kwenye hifadhi za taifa.

Naye Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Serengeti, Massana Mwishawa, alisema ujio wa kundi hilo kwenye hifadhi hiyo, utachangia kuongeza pato la taifa kupitia sekta ya utalii.

Mmoja wa wanawake wa UMAKI, Rachel Ngalya, aliipongeza serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuzilinda Hifadhi za Taifa kwa kuwa ni hazina kwa nchi.

"Tumefurahi sana kutembelea hifadhi hii, tumeona vitu vingi, tunaipongeza serikali ya Rais Samia kwa kuzilinda hifadhi hizi kwa kuwa ni hazina kwa nchi yetu, pia natoa wito kwa Watanzania wenzangu kutembelea vivutio nyetu kwa kuwa vipo kwa ajili yetu na siyo kwa wageni pekee," alisema Rachel.

# Meneja matatani kuondoa watu hifadhini bila kibali

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amemsimamisha kazi Meneja wa shamba la hifadhi ya Msitu Slayo Bukombe lililopo wilayani Chato mkoani Geita, Thadeus Shirima, kwa kufanya oparesheni ya kuwaondoa watu bila kuwa na kibali.

Dk. Ndumbaro, akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini hapa, alisema kuwa Meneja huyo anasimamishwa ili kupisha uchunguzi juu ya tuhuma zinazomkabili kwa kuwa hali hiyo imewasababishia wananchi hao kupoteza mali zao ikiwamo nyumba pamoja na mashamba.

Alisema kuwa, Wizara yake imepata malalamiko kutoka kwa Mbunge wa Bukombe pamoja na wabunge wengine kulalamikia oparesheni hiyo ambayo imeathiri wananchi wa eneo hilo.

Kadhalika, alisema kuwa wizara hiyo imeamua kumsimamiasha kazi meneja huyo na kumwagiza Katibu Mkuu kupeleka mtu mwingine atakayekwenda kushika nafasi hiyo.

"Oparesheni hazikatazwi, lakini lazima zizingatie kanuni, taratibu na miongozo, huyu yeye amefanya maamuzi (uamuzi)bila kushirikisha viongozi wake wa juu hata katibu mkuu ambaye ndiye kamanda wa haya mashamba yote hakuwa na taarifa yoyote juu ya oparesheni hiyo," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema kitendo cha kujichukulia madaraka mikononi ambacho amefanya meneja huyo kinaharibu sura ya Wizara hiyo pamoja na falsafa ya uongozi wa serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Oparesheni hii iliyofanywa bila kufuata utaratibu, sisi wizara hatuwezi kuifumbia macho kabisa lazima yoyote aliyehusika katika hili tutamshugulikia," alisema

Vile vile, alisema wizara imeshapeleka timu ya watu katika eneo la tukio ili kufanya tathmini ambayo itaainisha mambo mbalimbali ikiwamo athari kwa wananchi.

"Timu hii tumeipa muda wa wiki mbili ili ije na majibu ambayo yataonyesha kuwa ni chanzo cha tukio hili lakini pia hatari zilizotokea zimeathiri watu kwa kiasi gani ndipo tutatoa uamuzi wa mwisho,"alisisitiza Dk. Ndumbaro

Naye, Naibu Waziri Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema watumishi wote wanatakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni, taratibu na sheria na siyo vinginevyo.

"Sisi kama wizara hatutakuwa na nafasi ya kuwalinda wale wote ambao wanafanya kazi bila kuzingatia kanuni za utumishi wa umma na kufanya mambo kwa matakwa yao binafsi...katika hotuba ya bajeti waziri alieleza kuwa tayari watumishi zaidi ya 60, tumeshawafukuza kazi,"alisema Masanja

# Corona yaathiri urejeshaji wakimbizi makwao

**Na Christina Mwakangale**

TANZANIA imerejesha makwao wakimbizi 19,000 tangu Januari mwaka huu, huku ikielezwa kwamba uwapo wa ugonjwa wa Covid-19, kumesababisha kasi ndogo ya mchakato huo.

Mkurugenzi wa Idara ya Huduma kwa Wakimbizi, Wizara wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Sudi Mwakibasi, amesema Tanzania inahifadhi takriban wakimbizi 200,000 kwenye kambi tatu, ikiwamo Nyarugusu, Nduta na Mtendeli zilizopo mkoani Kigoma.

Mwakibasi aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wakimbizi jijini Dar es Salaam, ambayo kimataifa huadhimishwa Juni 20.

Alisema kwamba tangu 2017 nchi ilipoanza utaratibu wa kuwarejesha wakimbizi makwao, imewarejesha wakimbizi 129,000 kwa hiari, akisema matarajio ni kuendelea kufanya hivyo kulingana na hali itakavyoruhusu.

Mwakibasi alisema pamoja na kuwapokea wakimbizi kutoka nchi jirani na kuwahifadhi, vipaumbele vya serikali ni kuhakikisha usalama wao kwenye makambi, maandalizi ya kuwarejesha kwa hiari baada ya nchi walikotoka kupata suluhisho.

"Awamu wa kwanza ni wakimbizi 1,400 na ya pili ni idadi kama hiyo kwa wiki moja. Sera inasema wahifadhiwe katika makambi kwa sababu ni suala la muda. Sababu zilizowafanya wakimbie zikipata ufumbuzi na inapopatikana amani makwao, tunawarejesha," alisema Mwakibasi.

"Nisisitize wadau wa wakmibizi wasaidie suala la usalama kwenye makambi na hata na kuwarejesha makwao. Pia kuna uharibifu mkubwa wa mazingira kwenye makambi, sababu wanatumia kuni kupikia, jumuiya za kimataifa ziendelee kutusaidia, ili kufanikiwa kupatikana kwa nishati mbadala ili mazingira yasiendelee kuathiriwa."

Mwanazuoni wa Shule Kuu ya Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Khoti Kamanga, alisema duniani kuna watu milioni 82.4 waliopo nje ya nchi zao kutafuta hifadhi, kati yao milioni 26 wanatambulika kama wakimbizi rasmi.

Alisema Tanzania inaendelea kutambulika duniani kwa kupokea na kuhifadhi wakimbizi, tangu mwaka 1983 na kupewa tuzo ya heshima na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), kutambua mchango wa kuhifadhi wakimbizi.

UNHCR linasema takwimu za wakimbizi duniani huenda zikaongezeka mwaka huu, kutokana na janga la corona linalosababisha watu wengi kuyakimbia makazi yao.



Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara wa Vodacom Tanzania PLC, Linda Riwa, akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Itiso jijini Dodoma, baada ya kuzindua miamvuli inayozalisha nishati kwa kutumia jua mwishoni mwa wiki. Vodacom imezindua miamvuli hiyo kwa ajili ya kutunza mazingira na kuboresha maisha ya wanakijiji kwa kuwapatia umeme-jua kwa miamvuli hiyo kupata mwanga na kuchaji simu zao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Madiwani waonya watendaji upotevu fedha za makusanyo

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

BARAZA la Madiwani Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera limeonya watendaji wanaosababisha upotevu wa fedha za makusanyo ya ndani kwa kutoyafikisha benki.

Hayo yamebainishwa kwenye kikao cha kupokea na kujadili taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG), wakati wa majadiliano ya maoni ya Baraza hilo.

Akitoa maoni ya taarifa hiyo, Diwani wa Kata ya Bakoba, Shambani Rashid alisema, ukusanyaji wa mapato unafanywa na watendaji na kwa kipindi cha mwaka 2019/20, 2021 kiasi cha Sh. milioni 3.5 haikuingia benki.

"Kuna Shilingi milioni tatu pointi tano tunayoiona hapa haikuingia benki na unayonyesha ilikusanywa kwa njia ya POS hili litolewe onyo kali ili kurekebisha makosa yasijirudie kipindi kingine," alisema Rashid.

Diwani wa Kata Bilele, Theofiki Salumu alisema, ili kufanikiwa kwenye suala la fedha kuwapo na ushirikiano katika kusimamia mapato kwa kuunda kamati za fedha, elimu na nidhamu yenye kuwa na mkazo.

"Watumishi watambue sio lazima viongozi wa juu wafike kubaini udhaifu bali kutengeneza weledi na kupata hati Safi na fedha zionekane kupanua miradi," alisema Salumu.

Awali, akisoma taarifa mbele ya Baraza hilo, iliyopokelewa katika ofisi ya mkuu wa mkoa kutoka kwa CAG, Katibu Tawala wa Mkoa Kagera, Profesa Faustine Kamzora alisema, halmashauri sita ndani ya mkoa huo zimepata hati zinazoridhisha.

Kamzora alisema Manispaa ya Bukoba kwa mwaka 2019/20,20/21 haikuweza kupeleka kiasi cha Sh.milioni 256.4 kwenye miradi ya maendeleo.

Pia, upande wa fedha ya kinamama na vijana ambayo ni Sh. milioni 148.5 haikufanyiwa ufuatiliaji kutokana na muda wake kuisha.

## W/biashara minadani watakiwa kuchukua tahadhari ya corona

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Balozi Batilda Buriani, amewataka wananchi na wafanyabiashara katika mnada wa Ipuli kuchukua tahadhari ya kujikinga dhidi ya virusi vya corona.

Alisema ikiwa nchi jirani zinakabiliwa na tatizo hilo, ni vema kila mkazi wa Mkoa wa Tanzania akachukua hatua za kujikinga kama zinavyoshauriwa na wataalamu wa sekta ya afya.

Balozi Batilda alitoa kauli hiyo alipokuwa katika ziara ya kukagua ukusanyaji wa mapato na hatua zinazochukuliwa kwa wafanyabiashara wa ng'ombe , mbuzi na kondoo katika Mnada wa Ipuli uliopo Manispaa ya Tabora za kujikinga dhidi ya virusi vya corona.

Alisema ni lazima kwenye minada na maeneo yanayokusanya watu wengi kama vile sokoni , stendi , shuleni kukawekwa ndoo za maji tiririka, sabuni ili wanaofanya shughuli hapo waweze kunawa kila wakati.

Mkuu huyo wa mkoa aliongeza watu wote wanaoendesha shughuli za kujitafutia riziki katika Mnada wa Ipuli na maeneo yenye mikusanyiko kuvaa barakoa wakati wote na kutumia vitakasa mikono.

Katika hatua nyingine, mkuu huyo wa mkoa ameiagiza Idara ya Afya ya Manispaa ya Tabora kuhakikisha inajenga vyoo na kuboresha hali ya usafi katika Mnada wa Ipuli ili kulinda afya za watu wanakwenda siku ya Jumamosi kupata nyama choma.

Alisema hali ya usafi katika mnada huo hairidhishi na vyoo vilivyopo ni vichache ukilinganisha ya watu wanaokuwepo siku ya Jumamosi.

Aidha Balozi Batilda aliwaahidi wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo kutatua matatizo yanayowakabili ikiwamo la baadhi ya watu kuziba njia ya kupeleka ng'ombe mnadani , ukosefu wa majosho, ukosefu wa nyasi za kisasa za kulisha mifugo na ukosefu wa mbegu bora za ng'ombe

Awali mfanyabiashara wa ng'ombe, Haruna Mazoea, alisema wamelazimika kufuata ng'ombe wa mbegu kutoka Biharamulo mkoani Kagera na wengine nchini Rwanda kama njia ya kuboresha ng'ombe wa Tabora.

Alisema aina ya ngo'mbe kutoka Biharamulo wanafaida kwa kuwa ni wakubwa na wanauzwa kuanzia Sh.milioni 1.8 hadi 2 kwa mmoja.

HABARI KITAIFA

# Makalla ashauri watumishi kuepuka mikopo kandamizi

**Na Beatrice Moses**

WATUMISHI wa Umma nchini hususani walimu, wamekumbushwa umuhimu wa kukopa kwa malengo, sambamba na kuepuka mikopo kandamizi.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, na kubainisha kuwa, walimu na watumishi wengine wa umma wanapaswa kutambua umuhimu wa uwekezaji mdogo mdogo kwa ustawi wa maisha yao wawapo kazini na baada ya kustaafu na kutumia vema fursa za mikopo.

Makalla alitoa ushauri huo wakati akizindua kongamano la walimu na Benki ya NMB kwa mkoa wa Dar es Salaam 'Hatua kwa Hatua,', likiandaliwa na benki ya hiyo na kushirikisha walimu zaidi ya 300 toka wilaya za mkoa huo. "Tumieni falsafa ya 'I=C+S.' Maana yangu ni kuwa 'Income Can be Consumed or Saved.' Kwamba chochote unachopata unaweza kukitumia au kuweka akiba. Sasa tunakosea tunapogeuza pato lote kuwa 'Consuption.' Kadri unavyoweka akiba, ndivyo unavyoweza kufanya 'investment.'

"Ustawi wa maisha yenu ya sasa na baada ya kustaafu, unategemea uwekezaji mtakaofanya, ikiwamo kukopa kwa malengo, kuepuka mikopo kandamizi na kutotumia pesa za mikopo kwa anasa. Mimi mwenzenu ni shuhuda wa hili na niwaibie siri, ukiondoa NMB, taasisi nyingi za fedha hazina madirisha yanayokidhi mahitaji ya watumishi.

"NMB ndio benki kinara wa kuwakomboa watumishi wa umma, benki inayoongoza katika kubuni na kutoa huduma rafiki kwa walimu na watumishi wengine kwa kuwapa mikopo yenye riba na masharti nafuu. Walimu mna fursa pana ya kunufaika na benki hii," alisema Makalla.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alisema walimu ni kada muhimu miongoni mwa makundi yanayo hudumiwa na benki yake.

"Niseme tu kwamba, walimu ni kundi muhimu kwa benki yetu, ndio maana tumeandaa Siku ya Walimu na NMB. Kupitia siku hii, tunapata fursa ya kuongea nanyi, kutambulisha huduma mpya na kupokea mawazo mazuri kutoka kwenu, kwani nyie mnayaona mengi huko kwenye jamii na mawazo yenu yana thamani kubwa. "Majuzi NMB imekabidhi kwa serikali gawio la Sh. bilioni 21.8, mafanikio ambayo kimsingi yana mchango mkubwa wa walimu, kada ambayo bila uwapo wake, huenda NMB isingekuwa hapa ilipo. Ndio maana tuko makini kubuni huduma rafiki kwenu, zikiwamo za Kidijitali," alisema Mponzi.

Naye Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alisema NMB na Walimu ni jukwaa muhimu sio tu kwa kutoa elimu ya masuala ya fedha na kukusanya maoni yao, bali kunadi bidhaa mpya, ambako mwaka huu, pamoja na nyinginezo, wamekuja na Bima ya Vikundi.

Mwalimu Victor Timbuka wa Shule ya Msingi Msasani, wilayani Kinondoni, aliipongeza kwa namna inavyopambana kuwaelimisha walimu nchini masuala ya uwekaji akiba, huku alikiri kuvutiwa na kauli ya Makalla juu ya umuhimu wa kuweka akiba na kufanya uwekezaji mdogo kwa ustawi wa maisha yao ya sasa na baada ya kustaafu.



Mtaalamu wa Maabara wa Hospitali ya KAM Musika ya Kimara Korogwe jijini Dar es Salaam, Rosemary Shirima, akimtoa damu mmoja wa watu waliofika kwenye hospitali hiyo kwa ajili ya kupata huduma za bure za vipimo na matibabu kwenye kambi ya siku tatu ya kutoa matibabu bure ambapo watu 1,500 walipatiwa huduma hiyo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mzumbe inavyolikabili tatizo la ajira

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

CHUO Kikuu cha Mzumbe kilichopo mkoani Morogoro,kimeweka mkazo wa kutoa mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya kutoa wahitimu watakaoweza kutumia taaluma yao kujiajili badala ya kuzunguka na bahasha za vyeti katika maofisi kutafuta ajira.

Katika mpango wake Mzumbe imeanzisha kituo cha rasilimali ya kukuza mawazo ya ubunifu ambapo vijana wanaoendelea na masoko yao wanaanzisha shughuli za ujasiriamali, huku wakiendelea masomo yao.

Kauli hiyo ilitolewa na Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Lugano Kusiluka,wakati wa mahafali ndogo ya kwanza ya Chuo hicho yaliyofanyika katika kampasi kuu Morogoro.

Alisema pamoja chuo hicho kufundisha kozi mbalimbali, kimeweka mkazo huo pia wahitimu hao kukubalika kwenye sekta binafsi ambayo kwa sasa inapewa kipaumbele kwa ajili ya kuelekea uchumi wa viwanda ili wahitimu hao walete ushindani na ubora katika sekta hiyo.

" Hivi sasa Mzumbe imeweka mkazo mkubwa katika mafunzo kwa vitendo ili kutoa wahitimu wenye sifa na ubora wa wao kwanza kujiajili na sio kusubiri kuajiliwa "alisema Prof. Kusiluka.

Kadhalika, alisema wanaendesha miradi mbalimbali ukiwamo mkubwa wa Sh. bilioni 8.6 katika masuala ya afya ambao unashirikisha nchi wadau wa maendeleo.

Rais Mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ambaye ni Mkuu wa Chuo hicho, alitunuku shahada mbalimbali kwa mara ya kwanza tangu ateuliwe kushika wadhifa huo mwaka jana.

# Jafo aagiza mfumo majitaka kiwandani

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, ametoa miezi sita kwa kiwanda cha mifuko aina ya viroba kilichopo Chalinze kuhakikisha kinatengeneza mfumo wa majitaka.

Ametoa maagizo hayo kutokana na mfumo iliopo kutokuwa rasmi kwa utunzaji wa mazingira.

Jafo alitoa maelekezo hayo alipofanya ziara katika kiwanda hicho kujionea namna wanavyotunza mazingira.

Alisema kiwanda hicho kinatakiwa kutengeneza chemba ya mfumo wa majitaka kwa haraka tofauti na ilivyo sasa, ambapo hakuna mfumo wa utakatishaji maji.

Aidha aliagiza Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria kwa kiwanda hicho kutokana na hali iliyopo.

Pia alisema amekuwa akipokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusiana na uongozi wa kiwanda hicho kuchoma mifuko ambayo imekuwa ikitoa moshi mkali ambao una athari.

"Kuna malalamiko nimeyapata, hiki kiwanda muda huu pako safi hakuna moshi, ila kuanzia saa tano usiku wanachoma mifuko na moshi unaotoka hapa unaathiri wakazi wa maeneo ya karibu, NEMC njooni hapa kwa wakati wenu muangalie hatua gani za kuchukua," alisema Jafo.

Meneja wa NEMC Kanda ya Mashariki Kaskazini, Anord Mapinduzi, alisema amepokea maelekezo ya Waziri na watayafanyia kazi kwa wakati.

Naye msimamizi wa kiwanda hicho, Haji Abdallah, alihidi kutekeleza maelekezo ya Waziri Jafo kwa muda waliopewa.

Kabla ya kutembelea Kiwanda hicho, alikwenda katika kiwanda cha marumaru cha KEDA, na kueleza kuliridhishwa na mazingira ya mfumo wa majitaka na kuagiza viwanda vingine vikajifunze namna ya kutunza mazingira.

# ‘Mfumo kidigitali suluhisho huduma za kifedha vijijini’

**Na Mwandishi Wetu**

IMEELEZWA ili kuwafikia wananchi waliopo vijijini nchini, ipo haja ya huduma za kifedha kwa kutumia mfumo wa kidijitali ambao utarahisisha shughuli zao.

Nchini, watu waishio vijijini ni wengi, huku ripoti ya Benki ya Dunia (WB), ikionyesha asilimia 70 ya waishio huko chini ya asilimia 30 wana akaunti za benki.

Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Kibenki na Fedha kwa Misingi ya Kiislamu (AlHuda CIBE), Muhammad Mughal, alisema kutokana na hilo, wadau wa taasisi za kifedha watakutana kujadili umuhimu wa kuboresha, kutanua wigo wa huduma hizo katika misingi ya kiislam.

Alisema waishio mijini ni mara mbili ya idadi hiyo, huku asilimia 76 ya Watanzania wanaishi chini ya dola mbili kwa siku, wakati asilimia 75 wakiwa wamejiajiri katika sekta ya kilimo.

“Wadau katika sekta ya benki na uchumi kutoka Tanzania na nchi zingine za Afrika wanatarajia kukutana jijini Dar es Salaam mwezi ujao katika mkutano wa saba wa kimataifa kujadili fursa mbalimbali katika uchumi kwa misingi ya kiislamu.

“Mkutano huo utakaofanyika Julai 8, utajadili kwa kina umuhimu wa utoaji wa huduma za kibenki kwa misingi ya kiislamu (Islamic Banking) kwa maendeleo endelevu.

Alisema mkutano huo umefadhiliwa na ‘ICD and Codebase Technology’ Mikutano kadhaa kama hiyo iliandaliwa na kituo hicho miaka ya nyuma kwa nia ya kusaidia hali ya kiuchumi na kijamii kwenye maeneo ya vijijini na mijini.

“Mkutano utafuatiwa na midahalo na mafundisho kwenye utekelezaji wa misingi ya Kiislamu kwenye uendeshaji huduma za kibenki Julai 9 hadi 10. Zaidi ya wazungumzaji 15 wa kimataifa watatoa michango yao kwenye mada mbalimbali zitazozungumzwa,” alisema.

Mughal aliwashukuru wahisani kwa uaminifu wao kwao na mchango wao mkubwa walioutoa kwenye mkutano huu ili kuuwezesha kufanyika.

Alisema kuhifadhi fedha kwa misingi ya kiislam ndiyo njia mbadala wa kubadilisha maisha ya maskini. Kuwekeza katika mfumo wa kifedha na kibenki wa kiislam kutaleta uwekezaji mkubwa wa kigeni utaounganisha dunia, tengeneza ajira na kuboresha hali ya kijamii na kiuchumi na kuondoa umaskini.

# Wakili Msemwa: Niliwahi kulipwa mshahara wa mahindi na maharagwe

**Na Kulwa Mzaee**

WAKILI wa Kujitegemea, Jerome Msemwa, amesema katika utumishi kuna changamoto, hivyo uvumilivu unahitajika kwa kuwa aliwahi kulipwa mshahara mahindi na maharagwe baada ya fedha kukosekana.

Msemwa alisema hayo jana wakati wa hafla ya kutimiza miaka 25 ya uwakili, huku akijata kesi kadhaa ambazo aliwahi kushinda.

“Septemba 1993 niliajiliwa na Chama cha Ushirika Njoluma kama Mwanasheria wake hadi mwaka 1994 mwishoni nilipoacha kazi baada ya chama kuyumba sana kiuchumi, ilifikia mahala mshahara ulikuwa ukilipwa kwa kupewa mahindi na maharagwe mwishoni mwa mwezi,” alisema.

Alisema kipindi hiko kilikuwa kigumu kwake, kwani alikuwa ameoa na kubahatika kupata mtoto mmoja, Herry Jerome Msemwa. Wakili Msemwa alisema aliacha kazi na mwaka 1995 mwanzoni aliajiriwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kama Mwanasheria Msaidizi hadi Septemba mwaka 1996 alipoacha kazi kwa madai kuwa sababu ni mkuu wake kuwa mkali bila sababu na alikuwa anamuonea sana.

“Mwaka 1996 nilifuzu mitihani ya Sheria na kuapishwa na Jaji Mkuu Hayati Francis Nyalali kuwa Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania na mahakama zilizo chini yake, isipokuwa Mahakama ya Mwanzo.

“Kesi yangu ya mara ya kwanza katika maisha yangu ya uanasheria niliapa mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Jaji Mama Kileo katika shauri namba 7 la mwaka 1993, katika Mahakama Kuu Songea kesi hiyo ilikuja kusikilizwa katika Mahakama ya Njombe na Jaji J. L. Mwalusanya nilishinda

“Nikiwa wakili kamili wa kujitegemea, najivunia kumwalikisha mwandishi wa habari maarufu aliyefanyia katika vyombo vya habari vya ITV, Adam Mwibabile (marehemu) katika kesi ya jinai namba 17/1996 katika Mahakama ya Wilaya ya Songea akidaiwa kupokea nyaraka ya serikali kinyume cha sheria ya usalama wa Taifa ya 1970 ambapo alihukumiwa kwenda jela miezi 12, nilifungua rufani Mahakama Kuu , Jaji Dan Mapigano (marehemu) alimwachia huru.

“Nilimtetea na kuishinda serikali katika kesi ya Alhaji Shaban Mintanga, aliyekuwa anatuhumiwa kusafirisha dawa ya kulevya Mauritius, alikuwa Rais wa Chama cha Ngumi Tanzania na anadaiwa kusafirisha dawa za kulevya, Jaji Fauz Twaib alimuona mteja wangu hana hatia na akamuachia huru, nilifurahia ushindi huo,” alisema.



Mkuu wa Kitengo cha Biashara Benki ya NMB, Alex Mgeni, akizungumza na baadhi ya wafanyabiashara wa mikoa ya Kanda ya Kati, Dodoma na Singida walipokutana jana jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bohari kubwa ya mafuta kujengwa

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPUNI ya mafuta Kati ya Tanzania na Zambia(TAZAMA), inatarajia kukabidhi eneo ambalo litatumika kwa ajili ya ujenzi wa Bohari kubwa zaidi ya mafuta nchini kwa kampuni ya Kimataifa ya Dalbit na Kampuni ya Ujenzi ya BSL.

TAZAMA itakabidhi eneo hilo katika hafla maalum itakayoambana na uzinduzi wa ujenzi wa bohari hiyo.

Ofisa uendeshaji wa miundombinu katika kampuni hiyo ya BSL, Yucel Demirbas, alisema ujenzi wa Bohari hiyo utaleta mageuzi makubwa katika usambazaji wa mafuta nchini Zambia.

“Kwa sasa bidhaa ya mafuta ya petroli yanayosafirishwa kupitia Tanzania, yanahifadhiwa katika sehemu nyingi tofauti na jijini Dar es Salaam, hakuna sehemu moja yenye uwezo wa kutosha kutimiza mahitaji ya sasa, kwa hiyo wauzaji wa mafuta wanalazimika kulipa kampuni nyingi tofauti kwa ajili ya huduma za kuhifadhi mafuta na hivyo kuwaongezea gharama,” alisema Yucel.

“Bohari hiyo mpya itakayokuwa katika Wilaya ya Kigamboni ni suluhisho kwa changamoto hizi. Eneo lina uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 80,000 za dizeli na mita za ujazo 40,000 za petroli, ikimaanisha kuwa ina uwezo wa kuhifadhi mafuta yote yanayoelekea Zambia, hivyo kupunguza muda na gharama kwa wasambazaji wa mafuta. Itaongeza zaidi uwezo wa kuhifadhi, upatikanaji wa mafuta na kuondoa kero ya upungufu wa mafuta.”

Alisema ujenzi wa mradi huo ni wa miaka miwili na unatarajia kuanza rasmi Agosti mwaka huu na unatarajia kutoa ajira kwa Watanzania zaidi ya 250.

Pia, alisema utachangia ukuaji wa uwezo, ujuzi na teknolojia nchini, kukuza uchumi kwa serikali zote mbili za Tanzania na Zambia.

“Tuna furaha kubwa kuanza ujenzi wa mradi huu ambao utaleta mageuzi makubwa kwa uchumi wa Zambia na kutoa fursa za ajira kwa mamia ya Watanzania.Uhifadhi wa mafuta ni sehemu muhimu ya mfumo wa nishati kwa nchi yoyote ile, hivyo tunatarajia kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi zote mbili kwa kukamilisha mradi huu mkubwa unaounganisha serikali na sekta binafsi,” alisema Yucel.

“Na uzuri ni kwamba, hizi kampuni zinazoshirikiana katika mradi huu za Dalbit na BSL, zina historia nzuri ya utendaji nchini Tanzania na Zambia. Kwa Pamoja wamejenga jumla ya bohari tisa za mafuta tangu mwaka 2011, na kuongeza uwezo wa kuhifadhi mafuta kwa kiwango cha lita milioni 90.Miradi yao yote imekamilika kwa wakati, ndani ya gharama na bila matukio yoyote ya ajali kwa watendaji”

Nipashe
Spotika



VIUNGO 6 WANAOWEZA KUZIHAMA KLABU ZAO UK. 12 - 13

# REKODI 5 ZA MESSI AMBAZO RONALDO HAWEZI KUZIVUNJA

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi na Cristiano Ronaldo wamekuwa wakitawala soka la dunia kwa kipindi cha muongo mmoja na nusu sasa. Upinzani wao mkubwa kati yao umeibua mjadala mkubwa kwa mashabiki duniani. Ronaldo kwa sasa ana umri wa miaka 36, Messi akiwa na miaka 34 na wamejiwekea rekodi kadhaa katika miaka yao ya kucheza.

Lakini wachezaji hao wawili kwa sasa wanaonekana kama kipindi chao cha uchezaji kinaelekea mwisho.

Ronaldo na Messi ni wachezaji wawili ambao ni bora zaidi kwenye karne hii na wamekuwa wakitengeneza rekodi zao.

Makala haya yanaangalia rekodi za Messi ambazo Ronaldo hataweza kuzivunja, hizi hapa...

**#5. KIATU CHA DHAHABU ULAYA - 6**

Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya kinatolewa kwa mchezaji ambaye anafunga mabao mengi zaidi katika ligi kubwa tano Ulaya. Wakati Messi na Ronaldo walipokuwa kwenye viwango vyao vya juu vya kufunga mabao, walikuwa wanashindania Kiatu cha Dhahabu.

Ronaldo kwa mara ya kwanza alishinda tuzo hiyo akiwa Manchester United msimu wa 2007-08. Halafu akashinda tena mara tatu, msimu wa 2010-11, 2013-14 na 2014-15. Kwa wakati huo Ronaldo alikuwa akimuongoza Messi.

Lakini Messi alishinda katika misimu mitatu mfululizo kutoka 2016-17 hadi 2018-19. Sasa ameshinda mara sita tuzo ya Kiatu cha Dhahabu.

Robert Lewandowski alifunga mabao 41 kwa msimu wa 2020-21 na alitwaa Kiatu cha Dhahabu. Ronaldo alimaliza nafasi ya tatu msimu huu, huku Messi akiwa nafasi ya pili.

**#4. KUSHINDA MFULULIZO BALLON D'OR - 4**

Kutoka mwaka 2008 hadi 2019, ni Luka Modric pekee ndiye aliweza kuvunja utawala wa Messi na Ronaldo kushinda Ballon d'Or. Baada ya Ronaldo kushinda mara mbili mfululizo tuzo hiyo Messi akaja kushinda mara nne mfululizo kutoka mwaka 2009 hadi 2012.

**#3. MABAO MENGI KWA KLABU MOJA - 672**

Soka limebadilika sana kwa sasa na mchezaji mmoja kuichezea klabu moja kwa muda mrefu ni ngumu. Messi amecheza kwa kipindi chote cha maisha yake akiwa pale Barcelona. Ronaldo amecheza Sporting Lisbon, Manchester United, Real Madrid na Juventus.

Messi amefunga mabao 672 kwa Barcelona na aliivunja rekodi iliyowekwa na Pele ya kufunga mabao 643 katika klabu moja ya Santos.

Ronaldo amefunga mabao 450 katika mechi 438 kwa Real Madrid. Anashika nafasi ya 10 katika orodha ya wachezaji wenye mabao mengi zaidi kwa klabu moja. Ronaldo ndiye mchezaji pekee katika orodha hiyo ya wachezaji 10 ambaye bado anacheza.

**#2. MABAO MENGI KWA MWAKA - 91**

Kuna wakati Messi aliufanya mchezo wa soka kuonekana kuwa rahisi sana.

Wakati Messi akishinda kwa mara ya nne mfululizo tuzo ya Ballon d'Or mwaka 2012, alifunga mabao 91 kwa kipindi cha mwaka mmoja. Aliivunja rekodi ya Gerd Muller ya kufunga mabao 85 kwa mwaka mmoja. Na rekodi hiyo inaonekana itasimama kwa muda mrefu.

Ronaldo amefunga zaidi ya mabao 50 kwa mwaka mmoja mwaka 2017 na idadi hiyo ya mabao imekuwa ikishuka.

**#1. BALLON D'OR NYINGI - 6**

Messi kwa sasa anaongoza kwa kutwaa mara nyingi zaidi tuzo ya Ballon d'Or ambapo mwaka 2019 alitwaa kwa mara ya sita. Ronaldo ameshinda tuzo hiyo mara tano. Mwaka 2020 tuzo hiyo ilifutwa.

Kwa mwaka huu 2021, ni ngumu kutabiri nani atakayeshinda.

Lakini kwa sababu michuano ya Euro 2020 na Copa America 2020 inaendelea, bado kuna nafasi kati ya Messi na Ronaldo kuitwaa.

## ISIKUPITE

WACHEZAJI tisa waliofunga mabao mengi na kutoa pasi nyingi za mwisho tangu Januari Mosi, mwaka huu (katika mashindano yote kwa klabu na timu zao za taifa kwenye ligi kubwa tano Ulaya) ni Lionel Messi (30+10), Robert Lewandowski (34+4), Kylian Mbappe (29+5), Alberto Moreno (23+11), Memphis Depay (21+12), Erling Haaland (25+7), Cristiano Ronaldo (27+4), Antoine Griezmann (20+10) na Romelu Lukaku (21+9).



Extra Time



# VIUNGO 6 WANAOWEZA KUZIHAMA KLABU ZAO

**LONDON,** England

MICHUANO ya soka ya Mataifa ya Ulaya Euro 2020, ndio inayotawala kwa sasa, lakini klabu tayari zimeanza maandalizi kwa ajili ya msimu ujao.

**Dirisha la usajili litakuwa la aina yake, kwani klabu sasa zitakuwa na hofu ya kutumia fedha nyingi kwa ajili ya mchezaji mmoja, kutokana na mlipuko wa virusi vya corona kuzifanya timu kuyumba kifedha.**

Dirisha hili la usajili wa majira ya joto, linaweza kushuhudia viungo wakali wakiondoka katika klabu zao za sasa.

Kuna majina ya viungo wakubwa wakionekana kutaka kuondoka katika klabu zao, ingawa kuondoka kwao kunaweza kusiwe kwa fedha nyingi.

Makala haya yanawangalia viungo sita ambao wanaonekana wanaweza kuondoka kipindi hiki cha majira ya joto, hawa hapa...

### #6. GRANIT XHAKA

Muda wa Granit Xhaka pale Arsenal umegawanyika, na hivyo kuna uwezekano mkubwa akaondoka kipindi hiki.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alijiunga na Arsenal akitokea Borussia Monchengladbach mwaka 2016 kwa ada ya pauni milioni 40.5. Uwezo wake dimbani ukamfanya kupewa mikoba ya uongozi ndani ya kikosi hicho. Xhaka amekumbana na nyakati fulani mbaya kwa kushutumiwa na mashabiki wa Arsenal.

Raia huyo wa Uswisi ambaye amecheza mechi 220 katika mashindano yote kwa 'Washikabunduki' hao, amekuwa akihusishwa sana na AS Roma.

### #5. DONNY VAN DE BEEK

Msimu wa 2020-21, haukuwa mzuri sana kwa kiungo wa Uholanzi, Donny van de Beek. Baada ya kupata nafasi chache za kucheza pale Manchester United, majeraha yakamlazimisha kuondolewa kwenye kikosi cha Uholanzi kwenye michuano ya Euro 2020.

Ni zao la akademi ya Ajax, Van de Beek alikuwa mmoja wa wachezaji muhimu sana kwa timu wakati wa msimu wa 2018-19 wakati Ajax ilipofuzu kucheza nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Ni mchezaji mwenye akili na alijiunga na Man United kipindi cha majira ya joto kilichopita kwa dau la pauni milioni 35.

Alionekana kuwa ni mchezaji ambaye angeleta ushindani mkubwa kwa nyota kama Bruno Fernandes na Paul Pogba, lakini hilo halikutokea.

Van de Beek alianza katika mechi nne tu za Ligi Kuu England, akifunga bao moja na kutoa pasi ya mwisho moja. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, mara kwa mara amekuwa akitumiwa kama mchezaji wa akiba. Hivyo kwa sasa ni jambo la kusubiri kuona kama atakuwa kwenye mipango ya kocha Ole Gunnar Solskjaer msimu ujao. Van de Beek amekuwa akihusishwa na Inter Milan na Arsenal.

### #4. MIRALEM PJANIC

Moja ya usajili wa utata wa hivi karibuni ulitokea wakati Juventus na Barcelona walipoamua kubadilishana viungo. Arthur Melo alijiunga na miamba hao wa Serie A, huku Miralem Pjanic akisajiliwa kule Barcelona.

Msimu mmoja baadaye, ni sawa kabisa kusema kwamba, wachezaji wote wawili hawakuweza kufurahia misimu yao. Pjanic, ambaye alikuwa anachukuliwa kama mmoja wa viungo bora kabisa kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, hakuwa na nafasi sana kwa Barcelona, akianza katika mechi sita tu za LaLiga na akishindwa kufunga au kutoa pasi ya bao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, anajulikana kwa ubora wake na ufundi dimbani, amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kurudi Juventus. Huku Bayern Munich na Chelsea pia zimekuwa zinahusishwa naye.

### #3. JORGINHO

Mabadiliko yanaendelea kutokea kule Chelsea, huku kocha Thomas Tuchel akitaka kuimarisha kikosi chake ambacho bado kinaonekana kuwa bora.

Kiungo Jorginho, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Chelsea kwa muda sasa, anaweza kuondoka pale Stamford Bridge kipindi hiki cha majira ya joto. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia alikuwa nguzo muhimu zaidi kwa kikosi hicho cha Tuchel. Uzoefu wa Jorginho kwenye nafasi ya kiungo kuliifanya Chelsea kushinda Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hata hivyo, muda wa Jorginho unaonekana kuelekea mwisho.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye ameanza katika mechi 23 za Ligi Kuu msimu wa 2020-21, anatajwa kuwaniwa na klabu kama Juventus, Barcelona na timu yake ya zamani, Napoli.

### #2. MANUEL LOCATELLI

Halitakuwa jambo la kushangaza kuona Manuel Locatelli akiondoka kule Sassuolo kipindi hiki cha majira ya joto, hasa baada ya kuonyesha makali yake kwenye michuano hii ya Euro 2020.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia, amekuwa na kiwango cha aina yake kwa nchi yake kwenye hatua ya makundi ya mechi za Euro 2020. Alifunga mabao mawili wakati Italia ikishinda mchezo wa pili dhidi ya Uswisi. Hivyo Sassuolo inaweza kuamua kumuuza katika kipindi cha usajili.

Locatelli alianza katika mechi 32 za Serie A kwa Sassuolo msimu huu, akifunga mabao manne na kutoa pasi za mwisho mbili. Juventus na Manchester City zimekuwa zikihusishwa sana na kuwania saini yake.

Hivyo kuna uwezekano mkubwa akasajiliwa na klabu nyingine mara baada ya michuano ya Euro 2020.

### #1. PAUL POGBA

Paul Pogba kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuondoka Manchester United. Kipindi hiki cha majira ya joto kinaweza kumfanya aondoke klabuni hapo.

Mkataba wa Pogba na Manchester United unamalizika kipindi kijacho cha majira ya joto na hakuna ishara yoyote kama kiungo huyo anataka kusaini mkataba mpya.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, alikuwa kwenye kiwango cha kuvutia na nchi yake katika mchezo wa makundi wa michuano ya Euro 2020 dhidi ya Ujerumani, hivyo Manchester United inaweza kumuuza.

Maisha ya Pogba nchini England yamekuwa ya tofauti, angalau kwa kusema hivyo. Kiwango chake kimekuwa cha kupanda na kushuka, lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, amekuwa na wakati mgumu kwa kiwango chake kushuka na kupanda. Paris Saint-Germain na Juventus zinaonyesha nia ya kuwania saini ya kiungo huyo.

POGBA

## Nukuu

"Ni kweli mechi ilikuwa ngumu kwa pande zote mbili ila dakika za mwisho tulizembea, wenzetu wameanza mpira haraka, tumefungwa," **Nahodha wa Azam FC, Aggrey Morris, akizungumzia bao na mechi dhidi ya Simba wakati wakiangukia pua 1-0 kwenye mechi ya nusu fainali Kombe la FA**



"Tumekuwa tukifanya mazoezi ya penalti kwa kuongeza umakini kwa uwazi wa nini cha kufanya ikiwa hilo litatokea," **Beki wa England, John Stones kuelekea mechi ya hatua ya 16-bora Euro 2020 dhidi ya Ujerumani kesho.**



"Sababu moja kubwa zaidi ya kuondoka Chelsea ni kwa sababu yake [Jorginho] . Yeye ni mchezaji mzuri sana, mwenye akili, mpigaji pasi mzuri sana akiwa na mpira. Kitu pekee ninachoweza kusema juu yake wakati mwingine ni kwamba anaachilia mpira haraka sana wakati anapocheza mbele. Anaifanya timu kufanikiwa," **Kiungo wa Monaco, Cesc Fabregas.**





SONGNE

LUIS

# REKODI 7 KALI, SIMBA, YANGA KOMBE LA FA

**Na Adam Fungamwango**

YANGA ilianza kutangulia fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka nchini (TFF), maarufu Kombe la FA baada ya kuichapa Biashara United bao 1-0 kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora, Ijumaa.

**Jumamosi kwenye Uwanja wa Majimaji mjini Songea, Simba nayo ilitinga hatua hiyo kwa kuichapa Azam FC bao 1-0.**

Bao pekee la Yanga kwenye mechi hiyo ya nusu fainali lilifungwa na Yacouba Songne, huku Luis Miquissone naye akiipatia Simba bao pekee kwenye mechi ya nusu fainali ya pili.

Ni mechi mbili zilizovutia mno, achilia mbali uwanjani, hata mwamko tu wa mashabiki. Huenda ni kwa sababu TFF ilipeleka mechi hizo kwenye viwanja ambavyo kwa muda mrefu sana hazijachezwa mechi za Ligi Kuu.

Viwanja vyote vilijaa, mashabiki wa timu zote nne wakihanikiza na kuifanya michuano ya Kombe la FA msimu huu kuwa na mvuto wa aina ya pekee.

Kwenye makala haya, pamoja na mambo mengine tutaangalia baadhi ya rekodi na takwimu zilizowekwa na timu zote nne pamoja na wachezaji kwenye hatua hiyo ya nusu fainali...

## #1. YANGA YATINGA BAADA YA MIAKA MITANO

Yanga imetinga fainali hizo za Kombe la FA baada ya miaka mitano kupita. Mara ya mwisho ilikuwa mwaka 2016, ilipofanikiwa kuingia hatua hiyo na moja kwa moja ikaenda kutwaa kombe hilo kwa kuichapa Azam FC mabao 3-1 yaliyoyofungwa na Amissi Tambwe mawili na Deus Kaseke, huku bao la kufutia machozi la Azam likifungwa na Didier Kavumbagu.

## #2. SIMBA MARA MBILI MFULULIZO

Simba ndiyo mabingwa watetezi wa michuano hiyo. Msimu uliopita walitinga fainali kwa kuifunga Yanga mabao 4-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kisha ikaenda kulitwaa kombe hilo kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga kwa kuifunga Namungo FC mabao 2-1 kwenye mechi ya fainali. Msimu huu pia imetinga fainali baada ya kuidungua Azam FC bao 1-0.

## #3. BIASHARA YAWEKA REKODI MPYA

Biashara United imejiwekea rekodi ya kutinga hatua ya nusu fainali ya kombe hilo kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa. Ni timu iliyotokana na klabu ya Polisi Mara.

Timu hiyo yenye maskani yake mkoani Mara, ilipanda Ligi Kuu 2018, lakini kwa muda mfupi tu imeonekana kuwa tishio kwenye soka la Tanzania kwa sasa.

## #4. 'MCHAWI' WA AZAM NI SIMBA

Kwa misimu miwili mfululizo Azam FC imeshindwa kutinga hatua ya fainali ya michuano hiyo kutokana na kupata bahati mbaya ya kukutana na Simba.

Mara ya mwisho Azam kutinga hatua hiyo ilikuwa ni msimu wa 2018/19 na ikaenda kulitwaa kombe hilo kwa kuifunga Lipuli bao 1-0 kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi.

Msimu uliofuata ikakumbana na 'muziki' wa Simba kwenye hatua ya robo fainali na kuchapwa mabao 2-0. Kwa bahati mbaya sana tena msimu huu iliingia kwenye anga za Simba na kuchapwa bao 1-0.

## #5. WAGENI WAZIPELEKA FAINALI

Simba na Yanga zimetinga fainali kutokana na mabao yaliyofungwa na wachezaji wa kigeni. Raia wa Burkina Faso, Songne ndiye aliyeikatia tiketi Yanga ya kwenda kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma kucheza fainali, huku Simba ikitinga hatua hiyo kutokana na bao la raia wa Msumbiji, Miquissone.

## #6. NAMBA ZA DAKIKA ZA MABAO

Mabao yote ya Simba na Yanga yamefungwa kwenye dakika zenye namba zinazofanana. Bao la Yanga lilifungwa na Songne dakika ya 22 na lile la Miquissone lilifungwa dakika ya 88.

## #7. VIWANJA VYA DK. GAMA VYATIKISA

Viwanja vyote vilivyochezwa kwa miaka tofauti vilitikisa huko nyuma kutokana na kuwa na timu kali zilizoasisiwa na mmoja wa viongozi bora nchini waliokuwa wapenzi wakubwa wa michezo, Dk. Laurence Mtazama Gama.

Alipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, marehemu aliasisi timu ya Majimaji mwishoni mwa miaka ya 1970, iliyokuwa ikicheza mechi zake Uwanja wa Majimaji Songea ambao ndiyo ilichezewa mechi ya nusu fainali ya pili kati ya Simba dhidi ya Azam.

Dk. Gama, baada ya kuhamishwa kwenda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora miaka ya 1980, alikwenda kuasisi timu ya Milambo, ambayo nayo ilitikisa soka la Tanzania, ikicheza mechi zake kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi ambako ilichezewa mechi ya nusu fainali ya kwanza kati ya Yanga na Biashara United.

**JE, WAJUA?**



NGULI wa zamani wa soka, Alfredo Di Stefano, ambaye alifariki dunia Julai 2014, hadi sasa ndiye anayeshikilia rekodi ya kuzichezea timu za taifa tatu katika nyakati tofauti, akifanya hivyo kwa kuitumikia Hispania, Colombia na Argentina.





# TET yatakiwa kuzingatia maoni ya wadau uboreshaji wa mitaala

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI ya Baraza la Elimu Tanzania (TET), imeagizwa kuzingatia maoni ya wadau katika uboreshaji wa mitaala ya elimu ya awali, msingi na sekondari, ili kusaidia kuwa na wahitimu wenye uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki, alipokuwa akifungua mkutano wa wadau wa elimu kuhusu utoaji wa maoni ya uboresha mitaala hiyo.

Alisema bodi hiyo inapaswa kuwa makini na maoni yanayochangiwa ili kuwa na mitaala bora.

"Kama mtakumbuka kulikuwa na mchakato wa kuanzisha kufundisha somo la historia ambalo lingefundishwa kwa kiswahili kuanzia ngazi ya chini ya awali na kuendelea hadi vyuo vikuu, lakini hivi sasa unasubiriwa mchakato huu ukamilike ili kupata mtaala shirikishi na jumuishi utakaowezesha wahitimu kujiajiri na kuajiriwa," alisema.

Alisema kutokana na kuanza kwa mchakato huo, serikali imeona ni vema kuendelea na mtaala wa sasa.

"Katika karne ya 21 dunia imeshuhudia mapinduzi makubwa ya sayansi na teknolojia yaliyoleta utandawazi ambayo moja ya athari zake ni kuongeza ushindani katika soko la ajira, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha wahitimu wanapata ujuzi na maarifa utakaowawezesha kuwa na ufanisi katika soko la ajira ikiwamo kumudu maisha yao ya kila siku," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema mkutano huo ni muhimu kwa kuwa utawezesha wadau kutoa maoni ya uboreshaji wa mitaala ngazi ya elimu ya msingi ili kuwezesha wahitimu kuwa na stadi za ujuzi unaohitajika katika jamii.

Alisema mitaala bora ya ngazi hiyo itaweka misingi imara ya elimu kwa ngazi zinazofuata.

Aliwahakikishia wadau kuwa maoni yao yatafanyiwa uchambuzi wa kitaalamu kwa lengo la kupata mitaala bora itakayolenga ujuzi kwa wahitimu.

Alisema lengo la serikali ni kuwa na mitaala inayoendana na hali halisi ya kijamii, kisiasa kiuchumi sayansi na kiteknolojia ndani na nje ya nchi.

Naye, Katibu wa Wizara hiyo, Dk. Leonard Akwilapo, alisema serikali ya awamu ya sita imeweka msisitizo wa kuhakikisha kuwa na wahitimu wenye ujuzi ili kukidhi mahitaji katika ujenzi wa uchumi wa viwanda.



Katibu wa Taasisi ya The Dodoma General Muslim Association (DGMA)Twalib Mohamed Twalib (kulia), akionyesha hati na nyaraka za Shule ya Sekondari ya Jamhuri kuwa wao ndio wamiliki halali wa shule hiyo wakati alipozungumza na Waandishi wa habari mwisho wa wiki, kushoto ni mwenyekiti wa bodi ya Taasisi hiyo, Jamal Sharif Hussein. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Taasisi: Waislamu changamkieni fursa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAUMINI wa Kiislamu wa Mkoa wa Dodoma wametakiwa kuchangamkia fursa za kiuchumi zinazotolewa na taasisi mbalimbali za kifedha pamoja na asasi za kidini.

Katibu wa Taasisi ya The Dodoma General Muslim Association (DGMA), Twalib Mohamed Twalib alisema hayo wakati alipozungumza waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema fursa hizo zitawasaidia wao kujikwamua kiuchumi.

"Taasisi yetu inawaunganisha waisalmu wote Mkoani hapa hivyo waislamu wenzangu tuitumie kunufaika na huduma nyingi," alisema.

Kadhalika, alisema DGMA imekuwa ikifanya kazi katika Mkoa wa Dodoma pekee kwa kuwaunganisha Waislamu na kutetea maslahi yao.

Alitaja kazi zingine ni kuwaunganisha Waiislamu na taasisi za kifedha zinazotoa mikopo bila riba kwa sababu dini yao hairuhusu waumini wake kijiunga na taasisi zinazotoza riba kwa sababu ni dhambi.

Twalibu alisema taasisi hiyo kwa kushirikiana na vikundi vya wanawake wa dini hiyo wamefanikiwa kuwasaidia kuanzisha miradi ya kiuchumi katika maeneo yao.

Alisema DGMA inaendelea kutoa mafunzo kwa walimu wa dini shuleni kwa ajili ya kufundisha somo la dini kwenye shule binafsi na za serikali.

Aidha, alisema taasisi hiyo inamiliki mali nyingi ikiwamo shule ya sekondari ya Jamhuri iliyopo jijini hapa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) walipewa jukumu la uendeshaji ili kuwasaidia watoto wa kiislamu na dini zingine kupata elimu.

Alitaja mali zingine zinazomilikiwa na taasisi hiyo ni viwanja eneo la katikati ya mji wa Dodoma (maarufu majani ya chai) pamoja na viwanja eneo la Ihumwa Jijini hapa na Kibaigwa Wilaya ya Kongwa.

Alisema kiwanja cha Kibaigwa wanatarajia kujenga shule nyingine ambayo itatumika kutoa elimu katika jamii ili kutokomeza ujinga.

Alibanisha taasisi hiyo ipo kisheria na imesajiliwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi hivyo wananchi waitumie kwa maendeleo.

# Mhadhiri afichua tatizo kwenye ufundishaji

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa moja ya tatizo linalokabili sekta ya elimu ni namna ya kumfundisha mwanafunzi aelewe kwa lugha rahisi.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha St. John,Dk. Shadidu Ndossa, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika uzinduzi wa kitabu 'Language Supportive Pedagogy: Theory, Implementation and Application' uliofanyika kwa njia ya mtandao wa Zoom, jijini hapa.

Alisema ufundishaji ni namna ya kufundisha ili mwanafunzi kuelewa kwa lugha rahisi,inayoeleweka iliyojaa mifano rahisi, picha na vielelezo.

Dk. Ndossa alisema kutokana ufundishaji kuwa ni tatizo, walipata mradi wa Language Supporting Teaching and Text Book (LSTT) ambao ulikuwa na lengo la kumsaidia mwalimu kuweza kufundisha kwa lugha ya kueleweka.

Alisema kwa kupitia mradi huo wametunga vitabu vitatu vya kemia, baiolojia, na hisabati ambavyo vimekuwa msaada kwa wanafunzi na walimu.

"Wakati mradi kwa sasa unaelekea mwishoni na walimu nane kutoka katika mradi wameandika kitabu kutokana na kushiriki katika mradi huo,"alisema.

Aliongeza "Ni mradi ambao unahimiza mwalimu kutumia lugha au kuona lugha ni sehemu muhimu kuhakikisha wanafunzi wanaelewa hasa katika masomo ya Sayansi. Kwa mfano mimi katika chapter ambayo nimeiandika kama miongoni mwa waandishi niliandika kuelezea vile vitabu ni namna gani."

Alihimiza walimu kutumia lugha rahisi lugha inayoeleweka lugha iliyojaa mifano rahisi, lugha iliyojaa picha na vielelezo kuhakikisha mwanafunzi anaelewa dhana ambayo inafundishwa.

Naye, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) na kiongozi Mkuu wa Regional Education Learning Initiatives (RELI) Tanzania, Dk. Maryam Ismail, alipongeza waandishi wa kitabu huku akisema kimekuja wakati mwafaka kwa kuwa Tanznia ipo katika mchakato wa kupitia sera ya elimu.

"Tunaamini maarifa yaliyomo kitabuni yatachangia sana katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa watu wetu," alisema.

Kwa upande wake, Dk. Angeline Baret kutoka Chuo Kikuu cha Bristol cha Uingereza na Mtafiti Mkuu wa Mradi wa LSTT, alisema mradi umegusa wadau wengi na kuwajengea uwezo wa kujiamini walimu ili kufanya kazi kwa ufanisi.





## Taasisi, mbunge wachangia shule

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

TAASISI ya Tulia Trust inayoongozwa na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo la Rungwe, Anthony Mwantona, wamechangia mabati 72 kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Msingi Bagamoyo iliyopo wilayani Rungwe.

Shule hiyo inadaiwa kuwa haikuwahi kufanyiwa ukarabati tangu ilipojengwa mwaka 1934, hali iliyoifanya kuchakaa na baadhi ya majengo yake kuhatarisha maisha ya wanafunzi na walimu.

Katibu wa Mbunge Jimbo la Rungwe, Gabriel Mwakagenda, alisema mchango huo ulikuwa ni ahadi ya Mwantona ambaye aliahidi kuchangia, lakini akaamua kumshirikisha pia Dk. Tulia kupitia Taasisi yake ya Tulia Trust.

Alimpongeza diwani wa kata hiyo pamoja na wananchi wa Kijiji cha Bagamoyo kwa ushirikiano walioonyesha kwenye ukarabati wa shule hiyo kongwe.

"Niwapongeze sana wananchi wa eneo hili kwa kujitolea kwenye shughuli za maendeleo, kabla ya mchango huu mbunge alishachangia mabati 200 kupitia mfuko wa Jimbo kwa ajili ya miradi mbalimbali," alisema Mwakagenda.

Alimshukuru Naibu Spika, Dk. Tulia, ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kwa kumuunga mkono kwenye ukarabati wa shule hiyo na akawataka wananchi kuendelea kujitolea.

Naye Meneja wa Tulia Trust, Jacqueline Boaz, alisema msaada huo ni sehemu ya utaratibu wa taasisi hiyo kurudisha fadhila kwa wananchi na kwamba moja kati ya shughuli za Taasisi hiyo ni kuboresha sekta za elimu, afya na uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia mikopo yenye riba nafuu.

Aliwataka wadau wengine wa maendeleo mkoani humo kujitokeza kuisaidia shule hiyo pamoja na shule zingine ili wanafunzi wasome kwenye mazingira bora.

Akizungumza wakati wa kukabidhiwa mabati hayo mwishoni mwa wiki, Diwani wa Kata ya Bagamoyo, Kabuje Mtope, alisema wananchi wa Kijiji hicho kwa kushirikiana na wadau wengine walichangishana Sh. Milioni 2.5 kwa ajili ya ukarabati wa shule hiyo.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Joyce Mwangela, alisema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 315 kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba, na kwamba shule ina vyumba vya madarasa tisa vyenye uwezo wa kuchukua zaidi ya wanafunzi 500.

Alisema tatizo kubwa ambalo limekuwa likiikabili shule hiyo ni uchakavu wa vyumba vya madarasa, ambavyo alisema baadhi vina hali mbaya kutokana na kuta zake na mapaa kuchakaa.

# Maeneo mengi ya taasisi za dini hayana hatimiliki

**Na Nebart Msokwa, RUNGWE**

IMEELEZWA kuwa maeneo mengi yanayomilikiwa na Taasisi za dini mkoani Mbeya hayana hatimiliki za ardhi hali inayosababisha yavamiwe mara kwa mara na kuleta migogoro kati ya taasisi hizo na wananchi.

Hayo yalisemwa juzi wilayani Rungwe na Askofu Mkuu wa Kanisa la Pentecost Holiness Association Mission Tanzania (PHAMT) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi, Joseph Sichura, wakati wa ibada maalum ya kumsimika rasmi Askofu wa Kanisa hilo Jimbo la Rungwe, Methew Chawala.

Ibada hiyo ilifanyika katika Usharika wa Nazareth wilayani Rungwe na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kanisa hilo kutoka katika Jimbo la Nyanda za Juu Kusini Magharibi.

Kutokana na hali hiyo, Askofu Sichura, aliagiza viongozi wa kanisa hilo katika maeneo yote ya Jimbo hilo kuhakikisha wanafuatilia na kupata hatimiliki ya maeneo yote ya kanisa ili kuepusha migogoro hiyo ambayo alidai inakwamisha maendeleo ya kanisa.

Askofu Sichura alisema wakati makanisa hayo yanaanzishwa na wamishionari yalikuwa na maeneo makubwa, lakini kwa sasa baadhi ya maeneo hayo yameporwa na wananchi kwa sababu ya kutokuwa na hatimiliki za maeneo hayo.

"Mkakati tulionayo kwa sasa ni kuhakikisha maeneo yetu yote yanakatiwa hatimiliki, hii itatusaidia kupunguza migogoro inayotokea mara kwa mara kati yetu na jamii inayotuzunguka, sasa anayetakiwa kufuatilia hili ni nyie viongozi wa kanisa," alisema Askofu Sichura na kuongeza:

"Wakati huduma hii ya kiroho inaanza kutolewa hapa nchini, maeneo mengi yaliyojengwa makanisa yalikuwa yanatolewa bure na serikali pamoja na machifu wa maeneo haya, lakini kwa sasa yameanza kuchukuliwa na baadhi ya watu."

Kwa upande wake Askofu wa Jimbo la Rungwe aliyesimikwa kwenye ibada hiyo, Chawala, aliiomba serikali kupunguza masharti ya umilikishaji wa ardhi kwa taasisi za dini ili wapate hatimiliki za maeneo hayo haraka.

Alisema imekuwapo milolongo mirefu ya kumilikisha ardhi kwa maelezo kuwa baadhi ya watu wamekuwa wakikata tamaa ya kuendelea kufuatilia hati hizo kutokana na kuchoshwa na milolongo hiyo.

Chawala alisema Jimbo la Rungwe lina makanisa zaidi ya 70 na kati ya hayo, ni makanisa matatu pekee ndiyo yamekatiwa hatimili, hivyo atahakikisha katika uongozi wake anahamasisha wachungaji wa makanisa hayo wanapata hatimiliki ya maeneo yao.

"Rai yangu kwa Serikali itoe unafuu kwa taasisi za kidini kusiwe na mlolongo mrefu wa upatikanaji wa hatimiliki kama watu binafsi, na pia niiombe serikali itoe elimu ya umilikishaji wa ardhi, ili na wachungaji wakawafundishe waumini wao umuhimu wa kuwa na hatimiliki ya maeneo yao," alisema Chawala.

Mchungaji wa kanisa hilo Usharika wa Nazareth, Ambonisye Ndiga, alisema kuna athari kubwa ambayo kanisa limepata kutokana na kutokuwa na hatimiliki ya ardhi yao.

Alisema awali kanisa hilo lilikuwa na eneo lenye ukubwa wa hekta 20, lakini mpaka sasa limebakia na Hekta tano pekee baada ya hekta 15 kuporwa na wananchi.

Ndiga alisema eneo hilo walilipata mwaka 1948 wakati wanajenga kanisa hilo, na kwamba baadhi ya maeneo walikuwa wanalima na mengine walijenga miundombinu mbalimbali, na kwamba baadhi ya maeneo yaliyoporwa ni ambayo hayakuendelezwa.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Ulrich Matei, akiwaonyesha waandishi wa habari moja ya mashine zilizokuwa zinatumiwa na baadhi ya mawakala kusajili laini zilizokuwa zinatumika kwenye utapeli wa mitandaoni. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Elimu yaanza kuepusha mikopo umiza

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Mkoa wa Mbeya wameanza kupatiwa elimu itakayowasaidia kuepuka kuathiriwa na mikopo umiza ambayo imekuwa ikitolewa na taasisi za kukopesha fedha ambazo hazijasajiliwa na serikali.

Elimu hiyo imekuwa ikitolewa na Taasisi Isiyokuwa ya kiserikali ya Msaada wa Kisheria (LSF), yenye makao Makuu yake jijini Dar es Salaam na ina tawi katika eneo la Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (TEKU).

Maofisa wa Taasisi hiyo wamekuwa wakitoa elimu hiyo katika maeneo mbalimbali ya mikusanyiko ya watu ikiwamo kwenye vituo vya mabasi, vituo vya bodaboda na bajaji.

Akizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa utoaji wa elimu hiyo katika vituo vya mabasi vya Kabwe na Uyole, Meneja wa LSF, Aggripa Senka, alisema wananchi wengi wamejiingiza kwenye mikopo umiza bila kujua masharti ya mikopo hiyo.

Alisema kutokana na hali hiyo, wananchi hao wamekuwa wakijikuta katika wakati mgumu kutokana na wakopeshaji hao kuchukua mali zao zikiwamo nyumba, vyombo vya usafiri, mashamba pamoja na mali zingine kwa ajili ya kufidia mikopo hiyo.

"Mikopo hii imekuwa ya kilaghai, sana na wakati mwingine imekuwa ikisababisha migogoro kwenye familia, kutokana na baadhi ya wakopaji kutowashirikisha wenza wao, sasa sisi tunawaelimisha wananchi waiogope mikopo hii na badala yake wakakope kwenye taasisi zilizosajiliwa," alisema Senka.

Mkurugenzi wa LSF, Wakili Martha Gwalema, alisema katika kampeni hiyo wamefanikiwa kuwafikia wananchi wengi na kwamba katika maeneo yote waliyopita walikutana na wananchi ambao wameumizwa na mikopo hiyo.

Alisema baadhi ya wananchi waliochukua mikopo hiyo na mali zao kuchukuliwa walirejeshewa kwa ushirikiano kati ya Taasisi hiyo na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), na kwamba kurejeshwa kwa mali hizo ni sehemu ya mafanikio ya taasisi hiyo. "Katika maeneo tuliyopita tumebaini kuwa ni wananchi wengi wameumizwa na mikopo hii, mbali na kuwasaidia kurejeshewa mali zao pia tumewapatia elimu itakayowasaidia kuepuka mikopo hii," alisema Martha.

Kwa upande wake, Wakili Ezelina Mahenge, ambaye ni miongoni mwa waelimishaji, aliwaasa wananchi kabla ya kuingia mikataba ya mikopo hiyo wanapaswa kusoma kwa makini masharti, na kwamba ikiwezekana kuwatumia wanasheria kuwatafsiria masharti hayo.

Alisema ni vema wakopaji kushirikiana na wenza wao ama watu wao wa karibu ili kuepusha migogoro katika ndoa sambamba na kuzuia upotevu wa mali walizozihangaikia kwa muda mrefu.

Baadhi ya wananchi waliojitokeza kupata elimu hiyo ambao wengi walikuwa wanawake, walisema wengi ndoa zao zimeyumba kutokana na mikopo hiyo.

Mmoja wa wanawake hao, Subira Mwalembe alisema riba za mikopo hiyo ni kubwa, na imekuwa ikiwaumiza kwa maelezo kuwa wakikopa Sh. 50,000 wamekuwa wakilipa mpaka Sh. 1,000,000.

Mpaka sasa Taasisi ya LSF imewafikia zaidi ya wananchi 220,000 katika kipindi kisichozidi miezi sita.







Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ally Ame (wa kwaza kushoto), akikagua mradi wa ujenzi wa hoteli ya nyota tano akiwa na Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa, wa pili Mkurugenzi wa Kampuni ya Pannyroyal Limited Saleh Mohamed Said na wa tatu kushoto Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mahmoud. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# CCM yaridhishwa ujenzi hoteli nyota tano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Mapinduzi Mkoa Kaskazini Unguja (CCM), kimesema kimeridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa hoteli ya nyota tano unaotarajia kugharimu Dola za Marekani bilioni 1.6 licha ya kujitokeza tatizo la uhaba wa mchanga.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa CCM mkoa huo, Iddi Ally Ame, alipokuwa akifanya majumuhisho baada ya Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa kukamilisha ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi katika Kijiji cha Matemwe, Mbuyutende.

"Waheshimiwa wajumbe mimi naamini leo mmeona wenyewe watu hawa wapo makini na tumeridhika, naomba watu wa serikali kuwaunga mkono badala ya kuwakatisha tamaa wanapokuwa na matatizo ili kufanikisha mradi huu," alisema Mwenyekiti Ame.

Alisema mradi huo utasaidia kuongeza pato la taifa pamoja na kuzalisha ajira kwa vijana na kusaidia serikali katika utekelezaji wa mpango wa uchumi wa bluu chini ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussen Ali Mwinyi.

Hata hivyo, aliwataka vijana Katika Mkoa wa Kaskazini Unguja kutumia fursa ya ajira zinazoendelea kujitokeza kupitia miradi ya ujenzi ya hoteli za kitalii katika ukanda wa mashariki badala ya kuchagua kazi.

Alisema Rais mstaafu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, alikuwa na imani kubwa na mradi wa hoteli wa nyota tano wa 'Blue Amber' pia na Rais Dk. Mwinyi ana imani kubwa na mradi huo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohamed Mahmoud, alisema serikali imepitisha mradi huo lazima ukamilike kwa manufaa ya taifa na wananchi wa Zanzibar.

Ayoub alisema hoteli ya nyota tano inayojengwa katika Kijiji cha Matemwe Mbuyutende, itasaidia kuongeza ajira kutanua soko la biashara kupitia sekta ya utalii kwa wakulima, wavuvi, wafugaji na wajasiriamali pamoja na vikundi vya utamaduni.

Hata hivyo, Meneja wa mradi wa Kampuni ya Pannyroyal Limited, Murtaza Hassanal, alisema changamoto kubwa imejitokeza ya upatikanaji wa mchanga pamoja na kuathirika kwa shughuli za uchukuzi na usafirishaji wa mizigo kutoka nje ya nchi baada ya kujitokeza maradhi ya corona, mwaka jana.

Alisema awamu ya kwanza ya ujenzi inahitaji matumizi ya tani 15,000 za mchanga, lakini mpaka sasa wametumia tani 4,000 kutokana na serikali kuwapa kibali cha mchanga kati ya tani 300 mpaka 400 kila wanapoomba.

Hoteli ya nyota tano ya 'Blue Amber' inatarajiwa kuwa na nyumba za kuuza, vyumba vya hoteli, michezo ya baharini, uwanja wa gofu, maduka ya vyakula na ya vifaa vya utamaduni na awamu ya kwanza nyumba 60 zinatarajiwa kujengwa pamoja na vyumba 50

# Wananchi 327,000 kupata chanjo ya kipindupindu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WANANCHI 327,000 waliokuwapo katika shehia hatarishi ya uwapo wa ugonjwa wa kipindupindu Unguja na Pemba wanatarajiwa kupatiwa chanjo ili kujikinga na ugojwa wa kipindupindu.

Akizungumza katika mafunzo kwa waandishi wa habari, kuhusu chanjo hiyo, Ofisa kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), ambaye pia mratibu wa chanjo Zanzibar, Dk. Vendeline Simon, alisema chanjo hiyo ni miongoni mwa mpango wa mikakati ya kuondoa kipindupindu Zanzibar.

Alisema chanjo hiyo kwa awamu ya kwanza itahusisha shehia 58 ambazo ni waathirika wa mara kwa mara wa kipindupindu ikiwa ni mkakati wa kuondoa ugonjwa huo ifikapo mwaka 2028.

Naye Mkurugenzi Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Abdalla Suleiman, alisema chanjo hiyo ipo salama na tayari imeshatolewa katika nchi mbalimbali za bara la Afrika ikiwamo Tanzania.

Alisema chanjo hiyo inatolewa ikiwa ni sehemu ya tahadhari ya kupambana na ugonjwa wa kipindupindu ambao tayari umesababisha vifo vya wananchi 490 kwa nyakati tofauti.

Dk. Suleiman alisema chanjo hiyo ina uwezo mkubwa wa kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu na mtu atakayepata chanjo kamili atakuwa na uwezo wa kukabiliana na ugonjwa huo katika kipindi cha miaka mitatu.

"Zanzibar chanjo ya kipindupindu ilitolewa katika mwaka 2009 ambapo tangu kipindi hicho maeneo iliyotolewa chanjo hiyo hakuna matukio ya mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu," alisema.

Alisema chanjo hiyo itatolewa kwa njia ya matone katika awamu mbili tofauti na kwa upande wa Pemba jumla ya shehia tisa wananchi wake watapatiwa chanjo ikiwamo Chakechake na Wete.

# KMKM yatarajia kununua meli ya uvuvi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuelekea siku ya Kikosi cha Kupambana na Kuzuia magendo Zanzibar (KMKM), kinatarajia kununua meli ya uvuvi ambayo itatumika katika eneo la bahari kuu na kuvuna rasilimali zilizomo.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa kikosi hicho, Komodoo Azani Hassan Msingiri, wakati alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya kuanzishwa kwa kikosi hicho yanayotarajiwa kufanyika Julai mosi, mwaka huu.

Komadoo Msingiri, alisema kikosi hicho kimekabidhiwa majukumu makubwa ikiwamo ulinzi wa maeneo ya ukanda wa bahari, kukabiliana na uharamia unaofanywa na wavuvi haramu na kuharibu matumbawe (mazalia ya samaki).

Alisema wanatarajia kupata boti itakayofanya kazi za doria katika ukanda wa bahari ya eneo la kisiwa cha Unguja na Pemba ikiwa ni hatua ya kudhibiti matukio ya uvunaji wa rasilimali kinyume na sheria.

Alisema wanakusudia kununua meli ya uvuvi itakayofanya kazi ya kuvua katika maeneo ya bahari kuu ikiwa ni sehemu ya kuingiza mapato ya kikosi hicho.

"Hiyo ndiyo mikakati yetu na sehemu ya majukumu yetu kwa mujibu wa kuanzishwa kwa kikosi hichi kuona visiwa vya Unguja na Pemba vinakuwa salama katika eneo la ukanda wa bahari," alisema.

Alisema kikosi hicho kimekuwa na wigo mpana wa kusaidia jamii ndiyo maana hivi sasa wanahospitali ya kisasa ya kibweni na wananchi wengi wa Zanzibar wanaisafiria hospitali hiyo kwa ajili ya kupata matibabu.

Vile vile, alisema wakati umefika kwa wawekezaji kuwekeza Zanzibar katika miradi mbalimbali na Bahari iko salama na wakati wote kikosi hicho kinafanya kazi zake kwa weledi.

Alisema hivi sasa kikosi hicho kinafanya kazi kubwa ya kupambana na maharamia ambao wanatumia bahari kwa kusafirisha magendo hasa wanaotumia bandari bubu katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar.

Alieleza kuwa katika kuadhimisha siku ya KMKM, kikosi hicho kitakuwa na shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo kufanya usafi wa mazingira katika fukwe mbalimbali.

# Wazee walia kunyanyaswa upatikanaji huduma ya afya

**Na Steven William,** IRINGA

KUNDI la wazee wilayani Iringa lililopewa msamaha wa matibabu, limesema haliridhishwi na huduma za afya zinazotolewa kwa wazee hao katika hospitali ya wilaya hiyo na ya rufaa na kudai kunyanyaswa bila kupata dawa.

Wazee hao walimweleza Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, wakati akizungumza na wazee hao kujua kero zao mjini hapa.

Akitoa kero hiyo mkazi wa Iringa, Kelina Ungele, alisema serikali haijatilia mkazo suala la matibabu ya wazee kwa kuwa wanapata shida wanapofika hospitali na vitambulisho vyao vya msamaha na kuambiwa wakanunue dawa katika maduka ya dawa.

Mzee huyo alishauri ili kuondoa kero hiyo kwa wazee mkuu mpya wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo na jopo lake afanye mabadiliko ya tatizo hilo Wilaya ya Iringa.

Alisema kuwa kuna upungufu mkubwa katika hospitali za Wilaya ya Iringa kwa wazee kutopata dawa pamoja na kufika na vitambulisho vyao vya msamaha, badala yake wanapewa dawa za kutuliza maumivu (paracetamol) na nyingine wanaambiwa wakanunue za ugonjwa wanaoumwa.

Ungele alisema kuwa katika Hospitali ya Felimo, wajawazito wakitaka kujifungua kwa njia ya upasuaji wanaambiwa watoe Sh. 100,000 au 200,000 jambo linalowashangaza kwa kuwa huduma hiyo wanapatiwa bure.

Alisema serikali imetangaza mtoto chini ya miaka mitano anapougua anatakiwa apate matibabu bure, lakini wanatozwa fedha wanapopatiwa huduma ya matibabu.

Kwa upande wake, Lucas Mgongolwa, alisema kuna kero nyingine kubwa katika hospitali ya rufaa ya mkoa kugeuka kambi ya jeshi wananchi wanaokwenda kuwaona wagonjwa wao kunyanyashwa na askari wa wanaolinda lango kuu la kuingilia hospitalini hapo.

Alisema kuwa ndugu wanapochelewa kidogo muda wa kuingia hospitalini, askari wa getini wanawanyanyasa na wakati mwingine wanamwaga maji kwenye sakafu ili kuzuia wananchi kusubiri muda wa kuingia ndani kuwapelekea dawa ama chakula wagonjwa wao waliolazwa wodini.

Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ally Ngwada, alikiri kuwapo kwa upungufu huo na kuahidi kuendelea kuyashughulikia tatizo hilo.

Naye kwa upande wake alisema kuwa matatizo na kero za wazee hao atayashughulikia kwa kushirikiana na viongozi wenzake na kuwaomba wazee hao wampe baraka na ushirikiano katika uongozi wake.

Katibu wa UVCCM wilaya ya Iringa mjini Sayi Saamba, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Iringa, Steven Ngwale na Katibu Tawala Wilaya ya Iringa, Estomini Kiyando kwa nyakati tofauti walisema kuwa wazee hao wanakabiliwa na changamoto nyingi, lakini serikali imejipanga kutatua.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Dk. Philemon Sengati, akishiriki katika kuchimba shimo kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya choo cha Shule ya Sekondari Ngokoro iliyoko Manispaa ya Shinyanga kuadhimisha siku 100 za uongozi wa serikali ya awamu ya sita. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Jamii yatakiwa kurithisha watoto biashara

**Na Elisante John,** SINGIDA

JAMII nchini inayojishughulisha na biashara, imeaswa kurithisha mapema majukumu ya kazi kwa watoto wao, ili kuwajengea uwezo mapema na kuyaelewa mazingira ya kazi kwa wakati, kwa maslahi ya maisha yao ya baadaye na familia zao.

Ushauri huo ulitolewa jana na Meneja wa benki ya NMB, Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, wakati wa mkutano na wafanyabiashara wa matawi yaliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Itigi, Singida DC, Iramba, Ikungi, na Iramba Manispaa.

Alisema, tabia ya kurithisha kazi ya biashara watoto ni uamuzi sahihi unaopaswa kuigwa na jamii yote nchini, badala ya kuachwa mikononi mwa wafanyabiashara wenye asili ya Kiasia pekee.

"Tujitahidi sana kuwaandaa watoto wetu mapema kuwarithisha kazi ya biashara, na tukifanya hivyo tutawajengea msingi imara, ambao utawaimarisha kwenye majukumu ya biashara, watakapokuwa watu wazima," alisema Mlozi.

Alisema katika kipindi cha mwaka wa 2020, benki hiyo ilipata faida ya zaidi ya Sh. bilioni 206, zikiwa ni faida halisi baada ya kulipa kodi serikalini na zimetumika kwa ajili ya kuiletea jamii maendeleo.

Katika hatua nyingine, meneja huyo alifafanua kuwa kwa kipindi hicho pia mikopo mbalimbali ilitolewa kwa jamii yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni saba, kwa ajili ya kutekeleza shughuli na miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mlozi alisema kipindi hicho wakulima wakubwa, wadogo na wa kati, walikopeshwa zaidi ya Sh. bilioni 900, miundombinu ya nishati ya umeme na barabara zaidi ya Sh. bilioni 410, maji zaidi ya Sh. bilioni 550 na Sh. bilioni 140 kwa miradi mingine ya maendeleo.

Hata hivyo, meneja huyo alisema, benki hiyo inaangalia uwezekano wa kuwekeza kwenye ujenzi wa bomba la mafuta, linatoka nchini Uganda hadi Tanga (Tanzania).

# Watanzania washauriwa kupima afya mara kwa mara

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wameshauriwa kupima afya zao mara kwa mara ili kupeuka magonjwa kama sukari na shinikizo la damu ambayo yanaua watu wengi duniani kila siku.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Hospitali ya KAM Musika, Dk. Kandore Musika, kwenye kambi maalum ya matibabu bure kwa wananchi mbalimbali.

Hospitali hiyo iliyoko Kimara Korogwe, jijini Dar es Salaam, iliendesha kambi ya siku tatu na zaidi ya watu 1,500 walichunguzwa afya zao na kupatiwa matibabu bila malipo.

Dk. Musika alisema kwa kuwa hospitali hiyo ni mpya imejielekeza kutoa huduma zaidi kwa wananchi badala ya kuangalia biashara kwa kuwa Watanzania wengi hawawezi kumudu gharama za vipimo na matibabu.

Alisema kila mwaka Hospitali ya KAM Musika itakuwa ikitenga wiki maalum kwa Watanzania kwenda kufanyiwa vipimo na kupatiwa matibabu bure kama sehemu ya mchango wake kwa jamii.

Alisema kwenye kambi hiyo wamepima na kuwabaini watu mbalimbali wenye magonjwa kama uchafu kwenye njia ya mkojo (UTI), malaria, kuhara, sukari, shinikizo la damu na maradhi mbalimbali ya macho.

Alisema hospitali hiyo itajitahidi kuwasaidia Watanzania kwa kuhakikisha inawahudumia kwa gharama nafuu za vipimo na matibabu ili wengi wajitokeze kupima afya zao na kutibiwa.

Alisema ili kuepukana na maradhi mbalimbali pia wananchi wanashauriwa kula chakula chenye mlo kamili wenye protini, vitamini na wanga ili kuhakikisha wanakuwa na afya bora.

Alisema wanapaswa pia kusafisha mazingira ya kuishi kuhakikisha hakuna maji yanayotuama na ambayo hutengeneza mazalia ya mbu na kusababisha maradhi ya kuhara na kichocho.

Mmoja wa wanufaika wa matibabu hayo, Ndumaeli Ulomi, aliishukuru hospitali ya KAM kwa kutoa vipimo na matibabu ya bure akisema kuwa si Watanzania wote wanamudu huduma hizo.

# HABARI KIMATAIFA

## Bomu lajeruhi 2 kanisani DRC

**Beni,** DRC

WATU wawili wamejeruhiwa katika shambulizi la bomu ndani ya kanisa Katoliki katika mji wa Beni, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Mkuu wa Jeshi la Polisi mjini Beni, Narcisse Muteba Kashale, aliliambia shirika la habari la AFP kwamba, mlipuko huo umetokea saa 12 alfajiri jana, muda mfupi kabla ya shughuli ya sakramenti ya uthibitisho wa watoto kufanyika.

Kashale alisema, wataalamu wa Tume ya Amani ya Umoja wa Mataifa nchini Congo (MONUSCO), wamewafahamisha kuwa bomu la kutengenezwa nyumbani lilikuwa limetegwa hapo.

Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki mjini Beni, Laurent Sondirya, alithibitisha watu hao wamejeruhiwa katika mlipuko huo, kabla umati wa watu kukusanyika kwa hafla hiyo.

Sondirya alisema washambuliaji hao walilenga umati mkubwa wa watu kwa sababu hafla hiyo ingewaleta pamoja wazazi, watoto na waumini na misa haikuahirishwa. **DW**

## Trump akosoa utawala wa Biden

**Ohio,** MAREKANI

RAIS wa zamani wa Marekani Donald Trump, amezikosoa sera za uhamiaji za utawala wa sasa wa rais Joe Biden.

Akizungumza kwenye mkutano wake wa kwanza wa hadhara katika jimbo la Ohio, Trump aliwahimiza wafuasi wake kukiunga mkono na kukisaidia chama cha Republican kuwa na wingi na kulidhibiti bunge la Marekani, mwaka ujao.

Akiwahutubia maelfu ya wafuasi waliokuwa wakimshangilia, Trump aligusia baadhi ya orodha yake ya malalamiko, huku akikosoa uchaguzi wa Marekani na hasa kujikita katika ongezeko la idadi ya wahamiaji wanaoingia Marekani kupitia mpaka wa Kusini.

Kurejea kwa Trump katika mikutano mikubwa ya hadhara kunaanzisha mfululizo wa matukio ya hadhara kuwakosoa wanasiasa wa chama cha Republican, waliochaguliwa ambao anawaona walitofautiana naye.

Jimboni Ohio, Trump alimfanyia kampeni mpambe wa zamani wa Ikulu, Max Miller ambaye amezindua kampeni dhidi ya mbunge Anthony Gonzalles, mmoja wa wabunge 10 wa chama cha Republican, waliopiga kura kutaka Trump afunguliwe mashtaka kwa kuchochea shambulizi dhidi ya bunge la Januari 6, mwaka huu. **DW**

# Waziri afya Uingereza ajiuzulu kwa kuvunja sheria za corona

**London,** UINGEREZA

WAZIRI wa Afya wa Uingereza, Matt Hancock, amejiuzulu, baada ya kuvunja sheria ya kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona.


Inadaiwa hakusimamia kanuni ya kuweka mtu mmoja kati ya mwingine, akiwa na Msaidizi wake Mkuu Gina Coladangelo anayedaiwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi naye.

**Inadaiwa hakusimamia kanuni ya kuweka mtu mmoja kati ya mwingine, akiwa na Msaidizi wake.**

Gazeti la The Sun, lilichapisha picha zilizoonekana kumwonyesha Hancock na Coladangelo, wakibusiana katika ofisi moja ya wizara hiyo ya afya.

Katika barua yake ya kujiuzulu kwa Waziri Mkuu, Boris Johnson, Hancock alisema kuwa serikali ina wajibu kwa watu wake ambao wamejitolea pakubwa katika janga la virusi vya corona, kuwa waaminifu kwao wakati imewakosea.

Hancock aliongeza kuwa anataka kusisitiza ombi lake la msamaha kwa kuvunja mwongozo na kuiomba radhi familia na wapendwa wake, kwa tukio hilo na kwamba anahitaji kuwa na watoto wake kwa wakati huu. **DW**



Wafanyakazi wa idara tofauti za uokoaji, wakiendelea kutafuta manusura katika jengo la Champlain Towers South Condo, mjini Florida, nchini Marekani juzi. Jengo hilo liliporomoka mwishoni mwa wiki, hadi jana idadi ya vifo vimefikia vitano huku takribani 150 hawajulikani walipo. **PICHA: AP**

## Ripoti: Jengo lililoanguka lilititia tangu mwaka 1990

**New York,** MAREKANI

MHANDISI wa majengo, amesema aliona hitilafu ya nyufa na sehemu za kuta zinabomoka na nguzo dhaifu katika sehemu za kuegeshea magari zilizopo chini ya jengo la gorofa 13, lililoporomoka, jimbo la Florida, ripoti imesema.

Gazeti la New York Times la Marekani, liliripoti Jumamosi kwamba ripoti ya mhandisi wa majengo iliyotoka miaka mitatu iliyopita juu ya jengo lenye ghorofa 13 lenye makazi ya kuishi katika jimbo la Florida, huko Kusini mwa Marekani, ambalo lilianguka mwishoni mwa wiki, lilikuwa na kasoro na uharibifu mkubwa.

Mhandisi huyo aliona hitilafu ya nyufa na sehemu za kuta zinabomoka, nguzo zisizo imara katika sehemu za kuegeshea magari zilizopo chini ya jengo hilo, kulingana na gazeti hilo. The Times, lilisema kwamba ripoti hiyo ndio ilikuwa sababu ya kutayarisha ukarabati wa mamilioni ya dola ambao ulipangwa kuanza hivi karibuni.

Gazeti hilo lilisema, maofisa wa manispaa walitoa ripoti ya mhandisi mwishoni mwa Ijumaa.

Ripoti ya mwaka 2018, haikutoa ushahidi wowote kwamba jengo hilo lilikuwa karibu kuanguka, ingawa ilisema uharibifu kwa sehemu kubwa kwenye maeneo muhimu unahitajika kwa wakati.

Wakati huo huo, gazeti la Washington Post la Marekani, lilitoa mfano wa utafiti uliofanywa mwaka jana na kuripoti kuwa jengo hilo lilijengwa kwenye ardhi yenye unyevunyevu au maji, kwenye ukingo wa kisiwa ambacho kinaunda eneo la Miami Beach.

Taarifa iliongeza kwamba, jengo hilo limekuwa likititia tangu miaka ya 1990. Haijulikani bado ikiwa sababu hizo zilichangia tukio hilo kutokea. **VOA**

## UN yalaani mauaji wafanyakazi Tigray

**New York,** MAREKANI

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) Antonio Guterres amelaani vikali mauaji ya wafanyakazi watatu wa Shirika la Misaada la Madaktari wasio na Mipaka (MSF), yaliyofanyika huko Tigray nchini Ethiopia na kutaka wahusika wa mauaji hayo wakamatwe na kuchukuliwa hatua stahiki.

Kupitia taarifa yake aliyoitoa juzi, New York Guterres alisema "Nimeshtushwa sana na mauaji ya wafanyakazi hao, hii haikubaliki kabisa na ni ukiukwaji wa kutisha wa sheria za kimataifa za haki za kibinadamu. Wahusika lazima wapatikane na waadhibiwe vikali."

Guterres alituma salamu za pole na mshikamano kwa washirika wa UN, watoa huduma ya misaada ya kibinadamu ambao wanahatarisha maisha yao kwa kutoa ulinzi kwa watu wa Tigray. **UN**

# MULLER AMWOMBEA MABAYA KANE




**LONDON,** England

NYOTA wa Ujerumani, Thomas Muller, anatumai ukame wa kufunga mabao wa mshambuliaji Harry Kane wa England utaendelea kwa muda kidogo.

England inafufua upizani wao na Ujerumani kesho Jumanne wakati watakapokutana kwenye mchezo wa hatua ya 16-bora katika mashindano ya Euro 2020 kwenye dimba la Wembley, huku Kane akitarajia kuwaongoza 'Simba Watatu' hao.

Kane alianza katika mechi zote tatu za England za Kundi D, lakini hajafunga bao hadi sasa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, aliingia kwenye mashindano hayo akitoka kwenye wakati mzuri kule kwenye Ligi Kuu England akiwa na Tottenham akifunga mabao 23 na pasi za mwisho 14, lakini sasa ana wakati mgumu.

Hadi sasa amepiga mashuti matano, huku matatu yakionekana kuwa hatari na hakuna mchezaji aliyekosa nafasi nyingi zaidi ya hizo tatu za kwake.

"Washambuliaji wakubwa wanatakiwa kuwa wavumilivu," alisema Muller akiwaambia waandishi wa habari kuelekea mchezo huo.

"Straika mara zote anasubiria nafasi yake. Mara kwa mara anakuwa na mawasiliano na mpira.

# Mancini asifia mabadiliko, Italia ikifuzu robo fainali

**LONDON,** England

KOCHA wa timu ya Taifa ya Italia, Roberto Mancini, amesifia mabadiliko ya wachezaji ambao "walibadilisha mchezo" wakati Azzurri hao wakishinda 2-1 dhidi ya Austria kwenye muda wa ziada wa michuano ya Euro 2020 hatua ya 16-bora.

Federico Chiesa na Matteo Pessina wakitokea benchi waliingia na kila mmoja kufunga bao moja kwenye muda wa ziada, huku kuingia kwa Manuel Locatelli dakika ya 67 kulisaidia kubadilisha mchezo.

Mancini alianza kumuweka benchi Locatelli na kumuanzisha Marco Verratti, ambapo alipoingia alibadilisha kabisa mchezo huo na wakafanikiwa kutinga hatua ya robo fainali.

"Walikuwa kwenye kiwango cha kuvutia na hilo linaweza kuwa faida kubwa kwetu," alisema Mancini.

"Ukweli tuna wachezaji ambao wanaweza kubadilisha mchezo kwa sababu bado wanakuwa fiti na kwa hakika kilikuwa kiwango bora kabisa.

"Wachezaji walitaka kushinda kwa gharama yoyote na walifanya kazi nzuri na tulikuwa na uwezo wa kushinda."

Ushindi huo umewafaya Italia waendeleze rekodi ya kupoteza mchezo kufikia mechi 31, na kuzima ile ya mechi 30 chini Vittorio Pozzo kati ya mwaka 1935 na 1939.





# *Southgate kuongezwa mkataba mpya*

**LONDON,** England

CHAMA cha Soka cha England (FA), kimeamua kumuongezea mkataba mpya kocha wa timu ya taifa hilo, Gareth Southgate, baada ya mashindano ya Euro 2020, ni baada ya kuridhishwa na uwezo wake.

Southgate aliteuliwa kuwa kocha wa England Novemba 2016, akichukua mikoba ya Sam Allardyce.

Aliiongoza England kumaliza nafasi ya nne kwenye mashindano ya Kombe la Dunia mwaka 2018 kule Urusi na akapewa mkataba mwingine.

Na sasa FA imeona kuna haja ya kumuongeza tena mkataba mpya kocha huyo kutokana na kuifikisha timu hiyo katika raundi ya 16 ya mashindano ya Euro 2020, na kesho Jumanne watacheza na Ujerumani.

Southgate amekuwa akipingwa na wadau wengi wa soka la England kutokana na uamuzi wake wa upangaji wa kikosi na mbinu zake kwa ujumla.

HABARI MICHEZO

# PSG yafikia pazuri kumsajili Hakimi

**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Paris Saint-Germain, ipo karibu kukamilisha mpango wa kumsajili, Achraf Hakimi wa Inter Milan, kwa mujibu wa Jarida la France Football.

Mchezaji huyo raia wa Morocco mwenye umri wa miaka 22, alifurahia kampeni nzuri ya msimu wa 2020/21 akiwa na klabu hiyo ya Italia, akifunga mabao saba na kutoa usaidizi wa mabao 11 katika mechi 45 za mashindano yote.

PSG na Chelsea zinaendelea kuhusishwa na uhamisho wa nyota huyo hodari, ambaye ana uwezo wa kucheza kama kiungo na beki.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mwandishi wa habari wa Italia anayefanya kazi Sky Sport Italia, Fabrizio Romano, amenukuliwa na France Football kuwa, miamba hiyo ya Ufaransa ipo karibu zaidi na makubaliano na wanajiandaa kuwasilisha ofa ya mwisho katika siku zijazo.

Romano amedai kwamba, Chelsea bado inawasiliana na wakala wa Hakimi, lakini hawajatoa ofa rasmi kuomba huduma yake na hiyo imewafanya PSG kuwa kwenye nafasi nzuri ya kufanya yao.

Kijana huyo wa zamani wa Real Madrid, ambaye amebakiza miaka minne kumaliza mkataba wake pale San Siro, thamani yake inatajwa kuwa Euro milioni 80.







# MESSI CHANZO PANGA LA MISHAHARA BARCELONA

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA italazimika kupunguza bili ya mshahara kwa pauni milioni 171 ikiwa Lionel Messi atasaini mkataba mpya na klabu hiyo.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or alijaribu na akashindwa kulazimisha kuondoka mwaka jana, lakini Rais Joan Laporta anazidi kuwa na imani kwamba mkataba mpya unaweza kukubaliwa kabla ya msimu ujao.

Wakati Barcelona ikipambana na deni karibu Euro bilioni moja, klabu hiyo inazingatia kupata saini ya wachezaji huru kama Sergio Aguero, Memphis Depay na Eric Garcia wakati hali ya mkataba wa Messi ikipewa kipaumbele.

Kwa mujibu wa RAC1, Messi akisaini mkataba mpya atailazimisha Barcelona kupunguza pauni milioni 171 kwenye mishahara, ambayo inaweza kusababisha kuondoka kwa wachezaji kadhaa hapo Camp Nou.

Philippe Coutinho, Samuel Umtiti, Miralem Pjanic na Junior Firpo ni miongoni mwa wale ambao hatima yao haina uhakika hapo Catalunya.

Wakati nyota wawili wa Ufaransa, Antoine Griezmann na Ousmane Dembele, pia wamehusishwa na kuondoka katika wiki za hivi karibuni.

# *Varane akubali kutua Manchester United*

**MANCHESTER,** England

MLINZI wa Real Madrid, Rafael Varane, ameripotiwa kuikubalia Manchester United kujiunga nayo kuelekea msimu ujao 2021/22.

Kumekuwa na ripoti mbalimbali kuhusu uwezekano wa Varane kusajiliwa na United kwenye dirisha hili la usajili. Hii si mara ya kwanza kwa United kuhusishwa na Varane, mwaka 2011 ilibaki sehemu ndogo kumuona akitua pale Old Trafford, lakini mambo yalibadilika baada ya kupokea simu ya Zinedine Zidane, wakati ule alikuwa mshauri wa Florentino Perez.

Miaka takriban 10, Varane amekuwa Madrid na sasa ameweka wazi kwa uongozi wa klabu hiyo kuwa anataka kupata changamoto mpya na Ligi Kuu England ndio sehemu anayotaka kwenda.

Japokuwa kulikuwa na ripoti kuwa United walipeleka dau la pauni milioni 50 ambalo lilikataliwa na Madrid, Rais Perez amekanusha uhalisia wa kitendo hicho akisisitiza kuwa hawajapokea ofa yoyote inayomuhusu Varane.

Lengo kubwa la Madrid ni kumbakiza beki huyo kwa kumpa mkataba mpya ila kama anaweka wazi adhma ya kuondoka, huu ndio muda pekee ambao Madrid wanaweza kupata faida ya kumuuza Varane kabla hajaondoka kama mchezaji huru msimu ujao.

Changamoto kubwa inayoweza kutokea kwenye mchakato huu ni mshahara wa Varane. Inasemekana licha ya kuichagua United, Varane anataka mshahara wa pauni 400,000 kwa wiki. Huo utakuwa ni mshahara mkubwa kuliko mchezaji yeyote wa United.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# LIVER YAJITOSA MAZIMA KUMNG'OA MBAPPE PSG

## ●●● Klopp ni shabiki mkubwa wa Mbappe kama ilivyo kwa Rais wa Madrid, Perez, hivyo...

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imeripotiwa kuwasiliana na nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, juu ya mpango wa kutaka kumsajili, huku akiwa pia anawaniwa na Real Madrid.

**Mkataba wa sasa wa nyota huyo wa Ufaransa unaisha Juni mwakani na tayari Real Madrid walikuwa wanataka kuipata saini ya staa huyo katika dirisha hili la uhamisho baada ya michuano ya Euro 2020.**

Liverpool pia wamekuwa wakihusishwa na nyota huyo kwa kipindi cha miezi 12 sasa, na ripoti zinaeleza kuwa tayari wamewasilisha ombi la kufahamu ikiwa nyota huyu yuko wazi kuhamia klabu hiyo, kwa mujibu wa ESPN.

Taarifa zaidi zinasema kuwa Liverpool inayonolewa na kocha, Jurgen Klopp inaweza kulazimika kuwauza baadhi ya wachezaji, kabla ya kukamilisha uhamisho wa Mbappe.

Hata hivyo, ripoti zinaonyesha kuwa Mbappe mwenyewe anapendelea zaidi kuhamia Real Madrid, hivyo miamba hawa wa Hispania wanaonekana kuwa na nafasi nzuri zaidi ya kuinasa saini yake ikilinganishwa na Liverpool.

Wakati Mbappe mwenye umri wa miaka 22, akiwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake, kumekuwa na vuta nikuvute iliyopo katika mchakato huo, kwani mwenyewe anataka kuondoka hapo PSG msimu huu.

Kama Mbappe hatosaini mkataba mpya na PSG ina maana ifikapo Januari Mosi, 2022 ataruhusiwa kufanya mazungumzo na klabu yoyote nje ya Ufaransa, na kuna uwezekano akaondoka kama mchezaji huru.

Pamoja na hilo, PSG watapaswa kuingia sokoni kutafuta mbadala wake mapema iwezekanavyo.

Klopp ni shabiki mkubwa wa Mbappe kama ilivyo kwa rais wa Madrid, Florentino Perez.

Suala litakuja PSG kama wataamua kumuuza Mbappe basi gharama yake inaweza kuwa kuanzia pauni milioni 100 au zaidi.

## ZISIKUPITE

### COUNTINHO AGOMBEWA

PHILIPPE Coutinho anawaniwa na Inter Milan na Leicester, ambayo inanolewa na kocha wa zamani wa Liverpool, Brendan Rodgers na wanamtaka kwa mkopo. ***(Sport)***

### FOFANA ATUPIWA NDOANO

REAL Madrid inajiandaa kuwasilisha ombi la kuwasajili beki wa Leicester City na Ufaransa, Wesley Fofana, 20. ***(Star)***

### SANCHO SAFI MAN UNITED

JADON Sancho atapokea mshahara wa pauni 250,000 kwa wiki iwapo atakamilisha uhamisho wa kutua Manchester United, ikiwa ni zaidi ya mara mbili ya ule anaolipwa winga huyo wa England pale Borussia Dortmund kwa sasa. ***(Star)***

### MALEN KUMRITHI SANCHO

KLABU ya Borrusia Dortmund imesema kwamba, mshambuliaji wa PSV na Uholanzi, Donyell Malen, 22, ndiye mchezaji atakayechukua nafasi ya Jadon Sancho iwapo ataondoka katika klabu hiyo. ***(Mirror)***

### JAMES ATAKIWA CITY

MANCHESTER City imemuongeza nyota wa Chelsea na England, Reece James, 21, katika orodha ya wachezaji inayowawania, huku kocha Pep Guradiola akisemekana kummezea mate. ***(The Athletic)***

### COUTINHO AITAMANI LIVERPOOL

KIUNGO wa Barcelona, Philippe Coutinho, 29, ana ndoto ya kurudi katika klabu ya Liverpool, lakini 'Wekundu' hao wa Anfield hawana mpango wa kumrudisha raia huyo wa Brazil.

### VILLA YAJITOSA KWA ABRAHAM

ASTON Villa imejianda kuipatia ushindani Chelsea baada ya kuwasilisha ombi la pauni milioni 40 ili kumnunua mshambuliaji wa England, Tammy Abraham, 23, ambaye alifunga mabao 26 katika mechi 40 msimu wa 2018-19 akicheza hapo Villa Park.

### MADRID YAMUWANIA DALOT

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, anataka klabu hiyo ya Hispania kumsajili mlinzi wa Manchester United na Ureno, Diogo Dalot, 22, ambaye alihudumu msimu wa 2020 -21 kwa mkopo akiichezea AC Milan. ***(Correio de Manha via Sport Witness)***

### ZIYECH, GIROUD WANYATIWA

KLABU ya AC Milan ina hamu ya kuwasajili wachezaji watatu wa Chelsea, Hakim Ziyech mwenye umri wamiaka 28, na wachezaji wawili wa Ufaransa, Olivier Giroud, 34, na Tiemoue Bakayoko mwenye miaka 26. ***(Di Marzio via Sempre Milan)***

### DAKA HUYO LEICESTER

MSHAMBULIAJI wa Red Bull Salzburg, Patson Daka, 22, raia wa Zambia, amesema kwamba ameamua kujiunga na Leicester baada ya kufunga mabao 34 katika mashindano yote kawa msimu wa 2020-21.

## HABARI MICHEZO

# ABDULATIF ALIVYOIBUKA MSHINDI RAIS MPYA ZFF

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HATIMAYE mbio za kuwania Urais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), zimefikia ukingoni kwa Abdulatif Ali Yassin, jana kuibuka kidedea baada ya kuwabwaga washindani wake wanne waliokuwa wakiwania kiti hicho.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya ZFF, Fadhil Ramadhani Mberwa, jana alimtangaza Abdulatif kuwa mshindi wa nafasi hiyo ya juu kwa Shirikisho la Soka Zanzibar baada ya kupata kura 16 sawa na asilimia 67, akifuatiwa na Suleiman Shaban Suleiman aliyepata kura nane sawa na asilimia 33 kati ya kura zote 24 zilizopigwa katika uchaguzi huo mdogo uliofanyika kwenye Ukumbi wa Chuo cha Mafunzo visiwani hapa.

**Abdulatif alilazimika kusubiri kura kurudiwa kupigwa kwa mara ya pili jana ili kuibuka mshindi baada ya awali kutotimia asilimia 51 zinazohitajika kwa mujibu wa katiba.**

Katika kura zilizopigwa awamu ya kwanza, Abdulatif alipata kura 11, huku Suleiman Shabani Suleiman akipata kura Saba na Suleiman Mahmoud Jabir yeye akipata kura Sita huku wagombea wawili, Abdulkadir Mohmed Abdulkadir na Haji Shehe Hamad wakiambulia patupu.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, alisema kwa mujibu wa Katiba ya ZFF, upigaji kura unapaswa kurudiwa kwa mara ya pili, ndipo Abdulatif akaibuka mshindi wa uchaguzi huo kwa kupata kura 16 na Suleiman Shabani akipata nane na wengine wakitoka kapa.

Kwa matokeo hayo, sasa rais huyo mpya atapaswa kuchagua makamu wa rais kwa mujibu wa Katiba ya ZFF na kisha kuwasilisha jina katika mkutano mkuu ili lipitishwe.

Uchaguzi huo mdogo umefanyika kutokana na kujiuzulu kwa aliyekuwa Rais wa ZFF, Seif Kombo Pandu, mapema Februari, mwaka huu.

## IMEPITA HIYO...



Wanachama wa klabu ya Yanga wakipitisha mabadiliko ya katiba katika mkutano mkuu uliofanyika Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kikwete kuzindua Mr. UK Marathon

**Na Sabato Kasika**

RAIS mstaafu wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mbio za kwanza za MR. UK Marathon zitakazofanyika Julai 24, mwaka huu kwenye viwanja vya Leaders Club, Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Mbali na Kikwete, viongozi wengine watakaokuwapo ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Kitila Mkumbo.

Wanariadha zaidi ya 3000 wanatarajia kushiriki katika mbio hizo, ambazo zitahusisha zile za umbali wa kilomita 21, 10 na tano.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam, mratibu wa mbio hizo kutoka Mr. UK Sports Agency, George Damian, alisema Kikwete atazindua mbio hizo, ambapo kilomita tano zitahusisha viongozi mbalimbali, wakiwamo mawaziri.

Damian alisema, lengo la kuandaa mbio hizo ni kuchangia fedha kwa ajili ya matibabu ya watoto wenye maradhi ya mgongo wazi na kichwa kikubwa.

"Matarajio yetu kupitia mashindano hayo ni kuchangisha Sh. milioni 100, ili kurudisha tabasamu kwa watoto, ambao wamekuwa wakisumbuliwa na magonjwa haya yanayoenea kwa kasi barani Afrika na hapa kwetu Tanzania, na ukweli ni kwamba matatizo haya yanatibika," alisema Damian.

Kwa upande wa gharama za kushiriki mashindano hayo kwa wakimbiaji wa kilomita 21 na 10 watalipa Sh. 30,000, wakati wakimbiaji wa kilomita tano watalipia Sh. 20,000 na utaratibu maalumu wa kulipia umeandaliwa, ikiwamo mitandao ya simu kupitia namba ya MR. UK 5001515.

Kwa upande wa zawadi, washindi 10 wa kwanza kwenye mbio za kilomita 21 kwa wanawake na wanaume, kila mmoja atazawadiwa Sh. milioni moja, wakati mshindi wa pili akiibuka na Sh. 700,000, huku mshindi wa tatu akipata Sh. 500,000 na wa nne Sh. 300,000.

Alisema kwa wale watakaokimbia mbio za kilomita 10, kwa vikundi, washindi wa kwanza hadi wa tatu, watazawadiwa vikombe huku katika kilomita tano wapata zawadi ya fulana na medali.

Alifafanua kuwa, katika mashindano hayo kutakuwapo pia na burudani ya muziki ambapo bendi ya Malaika inayomilikiwa na Christian Bella inatarajiwa kutoa burudani sambamba na bendi ya muziki wa dansi ya Mapacha Watatu inayoongozwa na Jose Mara.

## Gomes: Azam wazuri ila Simba timu ngumu

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Didier Gomes (pichani chini), amesema alijua mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Azam itakuwa ngumu mno kutokana na uzuri wa timu wanayocheza nayo, lakini wao ni bora na wagumu zaidi.

Akizungumza kwenye Uwanja wa Majimaji mjini Songea mkoani Ruvuma juzi, kocha huyo alisema yeye, benchi la ufundi na wachezaji walijua kuwa mechi itakuwa ngumu na ikawa kama walivyotegemea, lakini anashukuru wachezaji wake walipambana na kujitolea hadi kupata ushindi.

"Kipindi cha kwanza tulijitahidi kucheza mpira wetu uliozoeleka, lakini ikawa vigumu. Kipindi cha pili tukaamua kucheza mipira mirefu na kumuingiza Meddie Kagere ili atusaidie kushambulia, lakini ilikuwa ngumu sana kuipita ngome ya Azam hadi dakika za mwisho. Azam ni wazuri, lakini sisi ni timu bora na ngumu," alisema Gomes.

Alisema amefurahishwa na ushindi huo na kuwapongeza wachezaji wake kwa kupambana hadi dakika za mwisho kwa nguvu ile ile.

"Malengo yetu ni kuchukua vikombe vyote. Ligi Kuu na Kombe la FA. Kwenye soka lolote linaweza kutokea, lakini hayo ndiyo malengo. Nawashukuru pia mashabiki wetu wa hapa wametupa ushirikiano mkubwa na kutushangilia sana, tunawaahidi tutaendelea kuwafurahisha," alisema kocha huyo.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Didier Bahati, alisema walipambana sana uwanjani, lakini bahati haikuwa yao.

"Niwapongeze Simba wamepata ushindi dakika za mwisho, ingawa nina mashaka na goli, mpigaji kama alipiga ndani ya boksi, na faulo ilichezwa nje ya boksi," alisema kocha huyo raia wa Burundi.



# Michezo

Jumatatu Juni 28, 2021

Nipashe




Liver yajitosa mazima kung'oa Mbappe UKURASA 22

NAWAAHIDI...




Mwenyekiti wa zamani wa Yanga, Yusuf Manji, akizungumza na wanachama wa klabu hiyo katika mkutano wao mkuu uliofanyika Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA PICHA: MTANDAO**

## Azam yakiri uzembe kufungwa bao Simba

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya wachezaji wa Azam FC, kuonekana kumzonga mwamuzi Ahmed Arajiga katika mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Simba wakionyesha kutokubaliana na bao lililofungwa na Luis Miquissone, nahodha wa timu hiyo, Aggrey Morris, alisema kuwa kilichowafanya kuadhibiwa ni kuzembea.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Majimaji mjini Songea, Simba ilibidi kusubiri hadi dakika ya 88, kupata bao hilo pekee la kuongoza baada ya Bernard Morrison kuchezewa madhambi nje kidogo ya 18 na kuipiga faulo haraka kwa Miquissone ambaye aliuzamisha mpira kimyani wakati wacheazaji wa Azam FC wakimfuata mwamuzi kupinga adhabu hiyo.

Baada ya bao hilo, wachezaji hao walizonga refa wakipinga bao hilo lakini Morris, akizungumzia mchezo na bao hilo alisema: "Ni kweli mechi ilikuwa ngumu kwa pande zote mbili ila dakika za mwisho tulizembea, wenzetu wameanza mpira haraka, tumefungwa."

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati: "Niwapongeze Simba wamepata ushindi dakika za mwisho, ingawa nina mashaka na goli, mpigaji kama alipiga ndani ya boksi, na faulo ilichezwa nje ya boksi."

# Nyota Yanga kuvuna bil. 4.9/-

## ●●● Wanachama wapitisha mchakato mabadiliko, Kikwete agusa usajili, Manji aahidi...

**Na Saada Akida**

KLABU ya Yanga imetenga kitita cha Sh. bilioni 4.9 kwa ajili ya kulipa mishahara kwa msimu wa 2021/22 huku pia ikitenga bajeti ya Sh. milioni 854.7 maalum kwa bonasi, imeelezwa.

**Mwenyekiti wa Yanga, Mshindo Msolla, ndiye aliyeanika suala hilo jana wakati akisoma bajeti ya klabu hiyo kwa msimu wa 2021/22 katika Mkutano Mkuu wa Wanachama uliofanyika jijini Dar es Salaam, maalum kwa ajili ya kuridhia mchakato wa mabadiliko ya katiba ili kwenda kwenye mabadiliko ya uendeshaji.**

Aidha, Msolla alisema Klabu ya Yanga imetenga jumla ya bajeti ya Sh. bilioni 7.9 kwa msimu wa 2021/22 ambapo katika bajeti hiyo, watakusanya Sh. bilioni 8.1 kutoka kwenye udhamini, jezi, mapato ya mlangoni, mitandao ya kijamii na ada za uanachama.

Msolla alifafanua kuwa katika udhamini, wamepanga kukusanya Sh. bilioni 4.9 wakati kwenye mapato ya jezi watakusanya Sh. milioni 350, ada za uanachama Sh. bilioni mbili, mapato ya mlangoni Sh. milioni 565 na katika mitandao ya kijamii Sh. milioni 960.

Katika mkutano huo ambao pia ulihudhuriwa na baadhi ya viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Baraza la Michezo nchini (BMT) na Wizara wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo huku Rais Mstaafu wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete akiwa mgeni rasmi, huku pia akiwapo Mwenyekiti wa zamani wa klabu hiyo, Yusuph Manji, kwa pamoja wanachama wa klabu hiyo waliridhia mabadiliko ya mfumo wa klabu hiyo kuendeshwa kisasa.

Msolla pia alitanganza wajumbe wa Baraza jipya la Wadhamini ambao ni George Mkuchika, Abbas Tarimba, Fatma Karume na Mwigulu Nchemba.

Baada ya hapo alipewa nafasi mgeni rasmi, Kikwete, ambapo aliwataka wanachama kuungana na viongozi katika jambo lenye kuleta maendelea katika klabu hiyo kuendeshwa kisasa.

"Wanachama mnatakiwa kutoa maoni mazuri ya kuitoa Yanga hapa ilipo na kusonga mbele hasa katika mchakato huu wa kipindi cha mabadiliko na klabu hii kuendeshwa kisasa.

"Wanachama kuweni na subira hasa katika mchakato mzima huu wa mabadiliko kwa kuonyesha utulivu na kuepukana na migogoro ambayo haina maana katika klabu," alisema Jakaya.

Kikwete aliwataka vingozi pia kuwa makini katika suala la usajili wa wachezaji na benchi la ufundi kuepuka kufanya mabadiliko ya kikosi kila msimu katika usajili wao.

"Tunatakiwa kuwapa muda wachezaji tunaowasajili na makocha tunaowaajiri kwa sababu hawawezi kutupa ubingwa kwa haraka lazima wakae pamoja na kuzoeana," alisema.

Aidha, Kikwete alisema Yanga inahitaji viongozi wenye uadilifu katika suala la kuweka wazi mapato na matumizi ya fedha za klabu hiyo, na kama itatokea kiongozi si muadilifu basi hafai kuiongoza.

Mwakilishi GSM ambao ni wadhamini wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said, alisema wataendelea kushikana bega kwa bega na klabu hiyo.

"GSM tutaendelea kuchangia fedha za kwenye usajili, kambi ya timu hiyo hata kama klabu itafanikiwa kuingia katika mchakato huo, tuwapo miongoni mwa hisa au la lakini tutaendelea kutoa mchango wetu," alisema Hersi.

Kwa upande wa Manji, alisema anashukuru kurudi nyumbani na mbele ya safari watazidi kushirikiana.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042